Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 76 No. 188 | SAF./RAB1. 1438 AH | JANUARI 2017 | SULH 1396 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini! Watu wasiwadhihaki watu wengine huenda wakawa ni bora kuliko wao; wala wanawake (wasiwadhihaki) wanawake huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msisingiziane wala msiitane kwa majina mabaya. Ni jambo baya sana kujichumia sifa mbaya baada ya imani; na wale wasiotubu hao ndio wadhalimu. (49:12)

Khalifa Mtukufu awatanabahisha wapinzani:

Islam Ahmadiyya Ishara ya Mbinguni

Na Mwandhisi wetu,
Dar es Salaam

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alitoa hotuba katika msikiti wa Baitul Futuh mjini London, ambapo aliwatahadharisha wapinzani ya Jamaat Ahmadiyya juu ya upinzano wao usio wa haki. Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema:

Wako watu ambao macho yao yamefungwa na ambao wameamua kwamba hawataamini wala hawatashuhudia juu ya Ishara za kweli za Allah. Kwa hakika hizi ni sifa na tabia za watu wasioamini mitume. Watu hawa hata baada ya kushuhudia Ishara lakini bado wataendelea kutaka ushuhuda zaidi ambao utakuwa sawa na fikira zao. Kwa sababu ya kuvuka kwao mipaka basi Allah ameifunga mioyo yao. Na kisha wameshindwa kuifikia imani.



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a.

Katika kipindi cha kudhihirisha ukweli wa Mitume wa Allah, Allah anawafaya watu hawa kuwa ishara ya kuasa na onyo kwa watu. Wapinzani wa Masih Aliyeahidiwa(a.s) nao pia walikuwa kama hivi. Watu hawa pamoja na kuona Ishara nyingi za kweli za Masih Aliyeahidiwa(a.s) lakini bado hawamuamini kwa sababu ya ukaidi na ubishi wao. Au wanaenda kinyume kabisa na zile ishara ambazo Allah amewaonyesha, basi Allah kwa hakika anawafaya wachache miongoni mwao kwa Ishara ya onyo.

Masih Aliyeahidiwa(a.s) aligusia ishara nyingi kuwa zilikuwa zinahusu ukweli wake na pia zilidhihirika kwa watu sawa na zile Ishara za Masih Aliyeahidiwa(a.s) ambazo zilielezwa na Mtume Mtukufu(s.a.w). Lakini viongozi mbalimbali wa dini wao wenyewe hawaziamini na pia wanawazuia watu wengine kuamini ukweli. Na wanaendelea kufanya hivi. Masih Aliyeahidiwa(a.s) mara nyingi, alitaja miujiza mbalimbali na Ishara za Allah ambazo zitadhirika juu ya ukweli wa Ahmadiyya. Alipokuwa anazitaja Ishara hizi alikuwa anasema kwamba ishara hizi zilielezwa na kutabiriwa na Mtukufu Mtume(s.a.w) miongoni mwa hizo ni kupatwa kwa jua na mwezi. Kama ishara hii isingetimia viongozi wa dini wangeonyesha hamaki na vurugu. Lakini pale ilipoonekana, sio mara moja tu bali ni mara mbili, mara ya kwanza ilikuwa India na mara ya pili ilikuwa Marekani, watu hawa walionyesha kuipuuza. Masih Aliyeahidiwa(a.s) alisema mmoja wa rafiki zangu alinieleza kuwa wakati Ishara hii ilipotimia, Ghulam Murtaza ambae alikuwa ni mmoja wa viongozi wa dini alionyeshwa kukatishwa tamaa sana na alionyesha kuumizwa sana na alitoa maoni yake kwamba sasa dunia inaenda kupotoka. Masih Aliyeahidiwa(a.s) akasema

Endelea uk. 3

Lukuvi: Naifahamu Jumuiya Ahmadiyya

Na Jamil Mwanga,
Dar es Salaam

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi amesema kuwa anaifahamu Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya tangu mwaka 1996 wakati alipohudhuria moja ya hafla iliyoandaliwa na Jumuiya Ahmadiyya ambapo marehemu Sebastian Kinyondo alialikwa kama mgeni rasmi.

Waziri Lukuvi aliyasema hayo ofisini kwake hivi karibuni alipokutana na uongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya ukiongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Mahmood Tahir Chaundry uliofika ili pamoja na mambo mengine, kumsalimia na kueleza shughuli zinazofanywa na Jumuiya ya Ahmadiyya nchini.



Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akikabidhi vitabu kwa Mh. William Lukuvi wakati alipomtembela ofisini kwake, Dar es Salaam

"Mwaka 1996 nikiwa Wizara ya Kazi nilikuja na marehemu Kinyondo, mlimpatia vitabu vingi ambapo alichukua likizo na vilimchukua siku saba kuvisoma vitabu vya Ahmadiyya, kisha akawaalika ofisini kwake kwa majadiliano akidai kuwa sasa ameshawafahamu" alisema, huku akicheka na kutabasamu.

Kwa upande wake, Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Mahmood Tahir Chaundry akiielezea Jumuiya ya Waislam Ahmadiya, alisema kuwa ni Jumuiya ya kidini yenye kiongozi mmoja duniani. "Ahmadiyya sio Jumuiya ya kisiasa, hatufanyi biashara na tunatii sheria za nchi", alisema na kuongeza kuwa Jumuiya Ahmadiyya imekuwa ikifanya mikutano ya mwaka

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KARIBU MWAKA 2017

Hotuba ya Ijumaa iliyotolewa na kiongozi wetu mpendwa Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) tarehe 30/12/2016 bila shaka itajipatia nafasi ya kipekee na ya kiheshima katika historia ya Jumuiyya ya Ahmadiyya. Kila neno la hotuba hiyo ni lulu yenye thamani na tunaomba kwa unyenyekevu mkubwa kila Muaminio atafute fursa ya kuisoma kwa makini na atafakari juu ya matone hayo ya asali yaliyomo katika hotuba hiyo.

Ni desturi ya binadamu kuanza mwaka mpya kwa mbwembwe na shamra shamra nyingi hadi kuwa kero na usumbufu kwa watu wengine. Furaha yako ikiwaletea maumivu watu wengine hiyo si furaha bali kayaya. Kiongozi wa Waaminio anataka tupeleke fikra zetu miezi 12 iliyopita. Je tulitimiza wajibu wetu sawasawa? Tulitekeleza masharti yaliyomo katika Baiat? Na kama tulipatikana na upungufu tumefanya nini ili kurekebisha upungufu huo? Mwanzo wa mwaka ni muda wa fikra nzito. Ni muda wa kujuta na kutathmini kuhusu ile shabaha kuu ambayo ni kumwabudu Allah na kutimiza wajibu wetu kwa viumbe wake. Mwanzoni mwa mwaka ni kukumbuka mahali gani tulipojikwaa. Na ni mahali gani tulipotumbukia katika shimo. Mwanzoni mwa mwaka unatakiwa uvae ile kanzu ya Mwaminio ambaye haanguki katika shimo lilelile mara mbili. Ukisha tathmini hayo yaliyopita kama anavyoshauri kiongozi wetu wa Waaminio ni jukumu lako kupiga moyo konde na kuahidi kuwa yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

Sehemu ya pili ya hotuba hiyo muhimu ni kujipanga ili uweze kufanya vizuri zaidi na kuhakikisha kuwa kila hatua yako ni ya kuelekea kwenye kutafuta radhi ya Allah. Katika kuelekea kwenye shabaha hiyo kiongozi wa Waaminio ametushauri yafuatayo:-

- **Kujiwekea ahadi ya kutofanya jambo lolote la kishirikina**
- **Kila siku iwe dhihirisho ya mfano bora wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw).**
- **Kutangaza umoja wa Allah**
- **Kujilinda na uongo na kutembea kwenye njia ya ukweli.**
- **Kujikinga na aina zote za uonevu.**
- **Kusimamisha sala tano kila siku.**
- **Kusali sala za Tahajjudi kila siku**
- **Kumsalia sana Mtukufu Mtume Muhammad (saw) (Darood)**
- **Kuendelea kuomba maghofira**
- **Kufuata amri zote za Qur'an Tukufu na mafundisho ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw).**
- **Kujiepusha na maneno ya kuudhi**
- **Kujiepusha kusambaza siri za wengine**
- **Kuwasamehe waliotukosea**
- **Kila kazi ianze kwa kumtukuza Allah**
- **Kujitolea kwa kazi za Jamaat**
- **Kujikinga kutazama mambo machafu kwa njia za mitandao na Runinga.**
- **Kuwakumbusha watoto wetu wawe watiifu kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) na kushikamana na kamba ya ukhalifa.**

Hata hivyo utamu wa dafu unywee maji humo humo kwenye dafu. Na utamu wa hotuba hii uisome mwenyewe na kuzingatia yaliyomo. *Mapenzi ya Mungu* inawatakia kheri ya mwaka mpya na mafanikio katika kutimiza hayo tuliyoagizwa na kiongozi wetu mpendwa.

Naifahamu Jumuiya Ahmadiyya

Kutoka uk. 1

(Jalsa Salana) kwa lengo la kukutana na kukumbushana masuala ya imani ambapo pia viongozi wa Serikali wamekuwa wakialikwa. Alisema kwa mfano, mwaka jana katika mkutano wa mwaka uliofanyika Kitonga, Dar es Salaam, rais mstaafu wa awamu ya pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi pamoja na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhandisi Hamad Yussuf Masauni walikuwa miongoni mwa wageni waalikwa. Aidha, alisema kwa takriban miaka sita sasa Jumuiya imekuwa ikiandaa mikutano ya amani nchini sawa na kauli mbiu isemayo: Amani kwa Wote bila chuki kwa yeyote.

Kuhusu shughuli za kijamii zinazofanywa na Jamaat Ahmadiyya nchini, Amir Sahib alisema kuwa mbali na huduma za afya na elimu kwa msaada wa taasisi ya 'Humanity First', Jumuiya Ahmadiyya imesaidia kuchimba visima na kuweka pampu za maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Kuhusu huduma ya maji, Waziri Lukuvi ambaye pia ni mbunge wa jimbo la Ismani mkoani Iringa alisema hata katika jimbo lake eneo la Izazi wapo waahmadiyya na kuiomba Jamaat iangalie uwezekano wa kufikisha huduma za visima vya maji katika eneo hilo.

Mwishoni, Amir na Mbashiri Mkuu alimkabidhi Waziri Lukuvi vitabu mbalimbali vya Jamaat Ahmadiyya ikiwemo tafsiri ya Qurani Tukufu kwa lugha ya Kiswahili kabla ya kupata picha ya pamoja na ujumbe wa Jamaat Ahmadiyya.



Picha ya pamoja kati ya Mh. Lukuvi na Amir Jamaat Ahmadiyya pamoja na msafara wake walipomtembelea

Makatibu wa Tahrik Jadid wa matawi ya Dar wajiwekea mikakati

Na mwandishi wetu,
Dares Salaam.

Baada ya kupata idhini ya Mheshimiwa Amir na Mbashiri Mkuu kikao cha makatibu wa Tahrik Jadid wa matawi ya Mkoa wa Dar es Salaam kilifanyika Kaluta House tarehe 14 Januari 2017 chini ya Uenyekiti wa Naib Raisi wa Mkoa Bwana Mustafa Abdu lmran. Makatibu kutoka matawi 16 walihudhuria kikao hicho ikiwa ni 59% ya matawi yote ya Dar es Salaam. Dar es salaam ina matawi 27 ya Jamaat. Pamoja na hao pia walihudhuria Naazim Tahrik Jadid Khudammul Ahmadiyya llaqa DSM, Mwalimu wa Zone na Katibu Taifa Tahrik Jadid.

Makatibu waliohudhuria na matawi yao kwenye mabano ni:- Luqmaan Jafar Malik Sahib (Magomeni Kagera). Mhando Mhina Sahib {Manzese Uzuri), Swalehe Kigumi Sahib (Mbagala Nzasa), Rahim Mwanga Sahib (Tegeta), Abdul Razzack Shoo Sahib (Safina), Kassim M. Maftah Sahib (Gongo Ia Mboto), Said Salim Mustafa Kapulilo Sahib (Kiwalani), Mohammed Mpambije Sahib (Chanika) na Aman lssa Mwakitalema Sahib (Amani). Wengine ni Nassir A Ndembo Sahib (Mnazi Mmoja), Jalaluddin M. Mbawala Sahib (Qadian), Ridhiwani A Muhimu Sahib (Temeke Mikoroshini), Ahmad Abdul Nasib Sahib (Magomeni Mikumi), Yahaya Mpate Sahib (Tabata). Fadhili A. Mshamu Sahib (Kitanga), Muhsin A. Kaye Sahib (Mabibo).

Viongozi wengine waliohudhuria ni Omari Mrisi Sahib (Naazim Tahrik Jadid Khudamul Ahmadiyya llaqa DSM), Mustafa Abdul lmran Sahib (Naib Raisi Mkoa wa DSM), Amiri K. Abedi Sahib (Katibu Taifa Tahrik Jadid} na Mwalimu Ali Salehe Hassan Sahib (Mwalimu wa Zoni ya Kinondoni). Picha ya pamoja ni ya washiriki hao na picha zingine ni za washiriki wakifuatilia kwa makini mjadala wa kikao hicho.

Hali ya washiriki ilionekana wazi kuwa ni watu wenye kutafuta Radhi ya Allah pekee kwa namna ya utulivu walikokuwa nao na jinsi ya uzungumzaji wao. Karibu kila mmoja alikuwa na jambo Ia kuchangia. Hakukuwa na posho ya kikao wala fedha ya usafiri kila mmoja alijitolea muda wake na fedha zake. Allah Awe radhi nao, Amin.

Mkutano ulianza saa 11. 15 jioni kwa usomaji wa Kuruani Tukufu na tafsiri iliyosomwa na Mwalimu Ali Salehe

Endelea uk. 5

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashirat Rahman
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Ahmadiyya Ishara ya Mbinguni

Kutoka uk. 1

hebu fikirieni kwamba, je yeye ndiye anayewatakia watu wema zaidi kuliko Allah?

Vilevile, tauni ni moja kati ya Ishara nyingi za adhabu ambazo zilitabiriwa. Pia kuna ishara za kutengenezwa kwa njia za usambazwaji wa maji, kukua kwa mawasiliano, kutawanywa kwa milima, taarifa nyingi za uchapishaji wa vyombo vya habari na maendeleo ya njia mpya za usafirishaji. Ingawa kuna bishara nyingi ambazo zilielezwa na Masih Aliyeahidiwa(a.s) zipo pia ambazo hazikutabiriwa na kuelezwa na Qurani tukufu na Mtukufu Mtume(s.a.w). Hazrat Musleh Maud(r.a) alisema kwamba watu hawa badala waangalie namna ambavyo ishara hizi zinavyotimia, wao wanaleta upinzani wa uongo dhidi ya Masih Aliyeahidiwa(a.s). Baadhi ya watu wanakuja na kusema kwamba Masih Aliyeahidiwa(a.s) kilemba chake hakikuwa sawa sawa hivyo anawezaje kuwa Masih Aliyeahidiwa(a.s)? Hazrat Musleh Maud(r.a) alisema Masih Aliyeahidiwa(a.s) aliwaonyesha watu hawa Ishara juu ya Ishara lakini watu hawa wanakuja na visingizio visivyokuwa na maana kabisa, kama vile hawezi kutamka vizuri herufi ya kiudru ya neno "Qaaf". Aliwaonyesha aya za Qurani tukufu juu ya aya lakini watu hawa wakasema atakuwaje Masih Aliyeahidiwa(a.s) kwa sababu yeye alimtengnezea mke wake dhahabu na anatumia mafuta ya mti wa lozi. Kisha Hazrat Musleh Mad(a.s) akasema msifumbe macho yenu katika bishara za kweli za Allah. Watu wengi walikuwa wakija kwa Masih Aliyeahidiwa(a.s) na kumuuliza juu ya Ishara zake. Naye Alikuwa anawajibu kwamba: Je, ulishawahi kufaidika na Ishara zangu za hapo kabla, mpaka sasa uhitaji ishara nyingine? Ikiwa hukufaidika na Ishara yoyote kati ya ishara elfu nilizozionyesha hapo kabla, je utafaidikaje ikiwa nitakupa ishara sasa hivi? Watu hawa watabakia kunyimwa baraka hadi mwisho wao.

Kuhusiana na ishara moja kubwa kabisa ambayo kila siku tunaishuhudia, Masih Aliyeahidiwa(a.s) alisema katika kitabu chake cha Barahin Ahmadiyya kuwa Allah amemfunulia dua hii "Usiniache peke yangu na utengeneze Jumuiya". Ufunuo mwingine uliotimia ni huu unaosema 'Allah atatimiza haja zako zote na watu watakujia kutoka sehemu za mbali'. Ufuno huu ulifunuliwa takribani miaka 26 iliyopita na unaendelea kutimia hadi leo hii kwa shani kubwa kabisa. Ishara hii ni Ishara ya mandeleo ya jamaat ambayo mpaka sasa inaendelea kutimia. Maendeleo ya jamaat zenu na kukua kwa utoaji wa michango ni moja kati ya njia kubwa kabisa zinazoonyesha ukweli wa Masih Aliyeahidiwa(a.s). Lakini Ishara hizi zinaweza kuonwa na wale tu ambao macho yao yapo wazi na sio vipofu.

Hazrat Musleh Maud(r.a) alisema Masih Aliyeahidiwa(a.s) aliambiwa na Allah mara nyingi kwamba Jamaat yako pia inatakiwa ijitolee katika njia kama zile zilizotumiwa na masahaba wa Mtukufu Mtume(s.a.w). Hivyo kujiona kwa Masih Aliyeahidiwa(a.s) anaingia katika nyumba iitwayo 'Nizaamu-ddin, maana ya Nizaamu-ddin ni njia ya dini. Njozi hii ilikuwa ina maanisha kuwa Jamaat Ahmadiyya siku moja itakuwa ndio njia ya pekee ya dini na itasimama na kuongoza mifumo mingine yote ya Dunia. In Shaa Allah.

Lakini maendeleo haya yatapatikana vipi? Kuhusiana na hili ilielezwa katika njozi kwamba baadhi yetu wataingia nyumba hii ya 'Nizaamu-ddin' kupitia njia ya 'Hassan' na baadhi wataingia katika nyumba hii kupitia njia ya 'Hussein'. Kila mmoja anafahamu kuwa mafanikio ya Hazrat Hassan(r.a) yalipatikana kupitia maelewano na mapatano na Hazrat Hussein(r.a) yalipatikana kupitia mateso. Hivyo, Masih Aliyeahidiwa(a.s) aliambiwa kuwa Jamaat itafikia katika kiwango cha 'Nizaamu-ddin' lakini wapo baadhi watafika kwa njia ya maelewano, mapatano na mapenzi na baadhi watafika kwa njia ya kujitoa na mateso. Ikiwa yupo mmoja wetu anayedhani kuwa Jumuia hii itapata maendeleo kupitia njia ya maelewano, mapatano na upendo tu basi huyo hayupo sahihi. Na ikiwa yupo anaefikiria kuwa Jamaat itaendelea bila ya watu kuteswa na kujitoa basi huyo pia hayupo sahihi. Maendeleo yetu yatapatikana kupitia njia za amani, mapenzi na pia kwa upande mwingine kupitia mateso. Hii inamaanisha kwamba tutajitolea maisha yetu (uhai wetu) lakini kamwe tusikate tamaa dhidi ya Imani yetu. Tunatakiwa tukanyage katika njia ya katikati. Baadhi ya maendeleo yatapatikana kwa njia ya amani na baadhi kwa njia ya mateso. Baadae Jamaat itaingia katika Nyumba ya 'Nizaamu-ddin' na itapata mafanikio. Hali zote hizi zinashuhudiwa na Jamaat. Amani, mapenzi na uvumilivu ndio ujumbe ambao Jamaat inausambaza na wakati huo huo Jamaat inajitolea.

Hazrat Musleh Maud(r.a) alisema mimi binafsi nilimuuliza maana ya ndoto hii Masih Aliyyeahidiwa(a.s) lakini alisema hajui kwa wakati ule, lakini maana yake imeendelea kujipambanua sawa na muda. Masih Aliyeahidiwa(a.s) katika wakati ule hakuwa na mtu hata mmoja aliyemuamini lakini Allah s.w. alimwabia Jamaat yako itapata maendeleo makubwa sana kiasi ya kwamba mataifa ya dunia yatakuja kwako kama wahamiaji katika zama hizi. Sisi ndio ambao tunashuhudia Ishara na Baraka za Allah kila siku na In Shaa Allah siku zinakuja ambazo tutapata maendeleo kiasi ya kwamba Jumuia nyingine zitaonekana kuwa ndogo, lakini ili kufikia maendeleo hayo ni lazima pia kuzalisha mageuzi ya kiroho na ya dini kwetu sisi wenyewe na vizazi vyetu. Tangu awali, jumuia za manabii wa Allah zinapata upinzani wa aina hii. Lakini upinzani huu hautufanyi sisi kuwa na hofu bali unatuongezea uimara katika imani zetu.

Siku chache zilizopita, viongozi wa Ofisi za Tahrik Jadid na Ziaul Islam press walivamiwa ghalfa na kitengo cha polisi kinachoshughulika na maswala ya Ugaidi huko Rabwah. Wabashiri wawili na maofisa wengine walikamatwa. Kuhusiana na tukio hili kuna baadhi ya watu wachache kutoka Rabwah wakiwemo kina mama waliniandikia kuwa 'Hatuhofii chochote kuhusu tukio hili bali tukio hili limetuongezea uimara katika imani zetu na imani zetu zimeongezeka zaidi baada ya tukio hilo na tuko tayari kutoa chochote na kukabiliana na ugumu wowote. Hii ndio hali inayotakiwa kuwepo kwa wanajamaat wetu.

Haya ni mambo ambayo yalielezwa na Masih Aliyeahidiwa(a.s). Kwa hakika ushindi wa mwisho utakuwa ni wa Jamaat ya Masih Aliyeahidiwa(a.s). Upinzani na uhasama, ulikuwepo na utaendelea kuwepo. Watu hawa wajinga ambao walianzisha mashambulio dhidi ya Jamaat ni kweli kabisa walifanyiwa ugaidi na Waahmadiyya kwa sababu Waahmadiyya walikuwa wanawaambia wawe na hofu ya Allah. Na ni nani ambaye anafanya ugaidi zaidi kuliko Yule anaewakumbusha wengine kuwa na hofu ya Allah. Hivyo wanataka kuwakamata Waahmadiyya na kuwaua. Allah awapatie busara ya kuelewa ukweli na Mwenyezi Mungu ailinde nchi dhidi ya watu hawa wenye misimamo mikali ya dini na viongozi wa dini ambao kusema haki ndio wamebeba maana ya ugaidi.

Hawa ndio wanaosambaza dhulma katika nchi na hakuna aliye salama kwa ajili yao. Allah awawezeshe kuwapa uimara kikosi hiki cha usimamizi wa Maswala ya Ugaidi kupambana dhidi ya watu wale ambao ni hatari kwa ajili ya taifa, ambao kiukweli halisi wanavunja mizizi ya amani ya nchi kwa kuteka watu nyara, badala ya kuwakamata Waahmadiyya ambao ni watu wa kupenda amani, na ambao ni watu wakweli wanaoitakia mema nchi yao na watu wa kutii sheria. Waahmadiyya wanatakiwa kuomba kwamba Allah ailinde Pakistan na ailinde dhidi ya dhulma na tabu dhidi ya viongozi hao (Ameen). Kama ilivyo katika hali ya kujitolea, Waahmadiyya wameendelea kujitolea na wataendelea kujitolea na Allah muda si mrefu atatupatia matunda yake. Vilevile katika nchi ya Algeria Waahmadiyya wamekuwa wanatendewa dhulma. Mwenyezi Mungu awalinde na awape uvumilivu dhidi ya ukatili huu na Allah aiwezeshe serikali yao kuelewa lengo la Waahmadiyya ambao kwa hakika ni watu wa amani na raia wazuri wanaotii sheria za nchi. Wanadaiwa kuwa wavunjifu wa amani na wanapanga mipango kinyume cha serikali, lakini katika dunia yote hakuna hata Ahmadiyya mmoja ambae ataonekana anapambana dhidi ya sheria za nchi. Sisi ni watu wa kusambaza amani, mapenzi na huruma na hatutasita kujitolea endapo kutahitajika ili kutimiza malengo haya. In Shaa Allah.

Hazrat Musleh Maud (ra) alisema kwamba hatari kubwa kupita zote na upinzani mkubwa kupita yote vinakuja kutoka kwa wenzetu na wenyeji. Hawawezi kuvumilia kwamba mtu fulani kutoka miongoni mwao aweze kupata heshima kiasi hicho na umuhimu katika dunia. Wale wanaopigana kwa ajili ya kila chembe ya mali dhidi yake, wanawezaje kuvumilia hali kwamba watu wengi kiasi hicho wanamfuata na kumuheshimu. Kwa hiyo wanajribu kila wanaloweza kumzima. Wale wanaokuwa hawajiwezi na hawawezi kufanya lolote, hata watu wa aina hiyo wanajaribu kutoa nje ya mioyo yao chuki kwa namna moja au nyingine.

Hazrat Khalifatul Masih I (ra) anasema kwamba mtu mmoja tajiri kutoka Shahpur alipata cheo cha 'Khan Bahadur'. Baada ya hapo mama mmoja masikini kutoka katika familia hiyo hiyo alimpa mtoto wake wa kiume jina la 'Khan Bahadur'. Alipoulizwa sababu alijibu kwamba sijui mtoto wangu atakuwa na utaalamu gani atakapokuwa mkubwa lakini angalau ataitwa kwa jina lile lile kama la yule mtu tajiri. Hivyo watu ambao hawawezi kufanya makubwa lakini wanapenda kuitwa kama wengine. Wakati Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alipodai kuwa ni Masihi Aliyeahidiwa wa zama hizi, mmoja kati ya ndugu zake pia alidai kuwa ni imamu Mahdi. Alifanya hivyo baada ya kuona kuwa watu wengi wanamfuata Masihi Aliyeahidiwa (as) hivyo na yeye wamfuate na awe wa muhimu hivyo hivyo. Hazrat Musleh Maud (ra) anatoa mfano wa Muajemi anayesema 'uwezo wa kila mtu wa kuwaza na kutafakari ni sawa na nguvu zake na mtizamo wake'.

Anasema kwamba Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alisema kwamba nimetumwa kuwa mtawala wa dunia yote na siyo kwamba inahitajika kwa watu masikini peke yao kuniamini bali pia kwa wafalme. Yule ndugu aliyedai kuwa ni imam mahdi alisema kwamba ametumwa kuwa kiongozi wa tabaka fulani la watu lakini Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alitaka hata mfalme wa Uingereza amfuate na hata alimuandikia barua. Yule ndugu aliyetoa madai ya uongo kuwa Imamu Mahdi alipopelekwa kituo cha polisi na kuulizwa kuhusu madai hayo aliruka kabisa madai hayo na akasema kwamba kuna mtu amemzushia hilo. Kwa hiyo, ndugu wa karibu ndio wapinzani wabaya zaidi kupita wote. Baada ya kusimulia tukio hili Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba tulikuwa na ndugu wengi ambao walitususa kwa sababu ya Ahmadiyyat. Sio kwa sababu hatukutaka kuonana nao lakini ni kwa sababu hawakupenda kuwasiliana nasi.

Ndugu zetu walikuwa wakitutukana. Shangazi yetu ambaye baadae aliikubali Ahmadiyya alikuwa akitunyanyasa. Hazrat Musleh Maud(as) anasema kwamba ninakumbuka kwamba wakati fulani nilipokuwa na umri wa miaka sita au saba hivi na nilikuwa napanda ngazi aliposema kwa kurudiarudia kwa kipanjabi 'mtoto kama baba kwa ubaya'. Alisema hayo mara nyingi sana kiasi kwamba ninayakumbuka vizuri na nikayasimulia nilipofika nyumbani na kuulizia maana yake. Huko Qadian Masihi Aliyeahidiwa (as) alipingwa. Hakuna mtu aliyeruhusiwa kwenda nyumbani kwake kwa ajili ya kazi yoyote au shughuli. Kaka zake wa karibu sana, shemeji na binamu wa kwa mama aliyeitwa Ali Sher walikuwa wakimjeruhi vibaya sana.

Siku moja katika eneo la Gujrat, marafiki wa Masihi Aliyeahidiwa (as) ambao walikuwa ni ndugu saba wote walikuja Qadian. Walikwenda kwenye bustani ya Masihi Aliyeahidiwa (as). Njiani ndugu yetu mmoja ambaye alikuwa anafanya kazi katika bustani yake aliuliza kuhusu kuja kwao Qadian. Walijibu kwamba tumekuja kutokea Gujrat kwa ajili tu ya Hazrat Mirza Sahib. Yule ndugu aliwaambia kwamba mimi ni binamu upande wa mama wa

Endelea uk. 4

Ahmadiyya Ishara ya Mbinguni

Kutoka uk. 3

Hazrat Mirza Sahib na ninajua fika ni mbaya kiasi gani alivyo! Aliposikia hivyo mmoja kati ya wale ndugu alimbana na aliwaita ndugu zake wengine. Yule ndugu akapata mashaka sana alipoona hivyo lakini yule muahmadiyya aliyembana akamwambia sitokupiga kwa sababu wewe ni ndugu wa Hazrat Mirza sahib. Ninataka tu kuwaonyesha ndugu zangu uso wako kwa sababu hata sasa tunasikia kuwa Shetani yuko lakini hatujawahi kuuona uso wake.

Kisha Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) aliambiwa na Allah kwamba ni nasaba yake tu ndiyo itaendelea na wengine wataisha. Hivi ndivyo hasa ilivyotokea. Sasa kutoka katika familia yake ni wale tu walioingia Ahmadiyya ndio wanaishi na vizazi vya wengine wote vimekoma na kuisha. Wakati Hazrat Mirza Sahib (as) alipodai kuwa Imam Mahdi wa zama, kulikuwa na takriban wanaume 70 kwenye familia. Lakini sasa kwa kuacha wale wanaohusiana na Masihi Aliyeahidiwa (as) kibaolojia au kiimani, hakuna hata mmoja wao aliye mtoto yeyote. Hawa ndio watu ambao walijitahidi kadri ya uwezo wao kulizima jina la Hazrat Sahib lakini matokeo yake wao wenyewe wameangamizwa na vizazi vyao havikukua. Hii pia ni moja ya ishara kubwa sana za ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa(as).

Wakati Hazrat Musleh Maud (ra) alipokuwa akisimulia tukio la baiyati ya 'Tayee Sahiba' anasema kwamba kuna baadhi ya tabiri na ushahidi ambao unawezekana kuonekana ni mdogo lakini unapofikiriwa kwa makini, maana zilizofichika ndani yao zinamsaidia mtu kukuza imani yake kwa kiasi kikubwa. Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba nilikuja jua kuhusu utabiri huu jana tu wakati wengine waliujua kabla. Jana wakati wa kifo cha 'Tayee Sahiba', Sheikh Yakuub Ali Sahib alieleza kwamba ni tabiri ya siku nyingi ya Masihi Aliyeahidiwa (as) kumhusu 'Tayee Ayee' . 'Tayee Ayee' alikuwa ni shangazi wa hazrat Musleh Maud (ra). Alikuwa ni mke wa kaka mkubwa wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Waahmadiyya wa zamani wanasimulia kwamba wakati hii inafunuliwa kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) ilikuwa ni vigimu kuelewa maana yake. Lakini maana nyepesi inayoweza kupatikana kutoka huo ni kwamba bibi ambaye ni shangazi yako (Tayee) kiundugu anakuja.

Maana ya kuja inaweza kuwa na tafsiri mbili. Moja ni kwamba anakuja karibu au nyingine ni kwamba anajiunga na Jamaat Ahmadiyya. Kuja tu hakuwezi kuwa ni utabiri wowote kwa sababu ndugu mara nyingi huwa wanakuja. Katika familia yetu, hata wazee wengi huwa wanamuita mke wa kaka mkubwa wa Hazrat Mirza Sahib(as) kuwa 'Tayee'. Hivyo jina lake lilikuwa ni 'Tayee'. Watu waliosoma vitabu kuhusiana na Ahmadiyya wanaujua ukweli kwamba 'Tayee' alikuwa ni mpinzani mkali wakati wa utabiri wa 'Mohammad Begum'. Kwa kuwa alikuwa ni mkubwa katika familia na utabiri ulimuhusu mpwa wake (binti ya dada yake), kwa hiyo aliona ni lazima kwake kuvunja undugu huu kwa kuwa aliona hilo ni fedheha kwa familia hiyo. Kwa mtazamo wake ilikuwa ni lazima kwake kuufanyia kazi. Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba kutokana na asili ya wanawake, kwa mwanamke mkubwa katika familia, heshima ya familia na hadhi ni ya juu kushinda masuala yote ya kidini na kwa kweli masuala yote ya kisiasa. Wakati huo, dai la Hazrat Sahib (as) kuwa ni Masihi Aliyeahidiwa halikuwa la muhimu kama ilivyo 'Tayee' kwa familia. 'Tayee' sahiba alijiona kuwa yu mkarimu kwa Masihi Aliyeahidiwa kwa sababu alikuwa mkubwa ki umri na pili alikuwa akimpelekea chakula cha mchana na cha usiku kwa kuwa hakudai sehemu yake ya mali. Wanawake kwa kawaida huwa wana hisia za aina hii kwa hiyo anajiona kuwa yeye ndiye mwenye kumlea Masihi Aliyeahidiwa (as).

Masihi Aliyeahidiwa anasema katika moja ya beti zake za ushairi za kiarabu kwamba 'kulikuwa na wakati ambapo nilikuwa nawategemea wengine kwa ajili ya chakula lakini sasa Allah Amenibariki kwa ile hadhi kwamba watu wengi wanakula chakula kutoka katika jiko langu'. Katika ubeti huu ni dhahiri pia kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) sio tu kwamba hakudai sehemu yake ya mali bali alimpa hiyo kaka yake. Baba wa Masihi Aliyeahidiwa (as) pia alikuwa akisema kuwa hataweza kuihudumia mali. Kwa hiyo kwa kuangalia hali zote za kifamilia, ilikuwa haiwezekani kwa 'Tayee' kuingia duara la Ahmadiyyat. Baadae alikuja kuikubali Ahmadiyyat.

Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba haikuwa kwa hoja au sababu za kidini bali kutokana na hali ya kifamilia, alijiona yeye kuwa ndiye mmiliki na Masihi Aliyeahidiwa (as) kuwa mtumishi (audhubiLlallah). Alimuona (Masihi AS) kuwa ni mtu masikini ambaye asingeweza kufanya kazi na kwamba (Masihi AS) ataishi kwa chakula chake (huyo bibi). Katika hali za namna hii, ilikuwa kamwe haikubaliki kwake kwamba amuoe mpwa wake. Kwa kuwa alikuwa ndiye mkubwa katika familia basi ilimpasa kulipinga suala hilo kupita yeyote. Katika wakati ule, upinzani ulikuwa umefikia kilele chake. Ndugu wa Masihi Aliyeahidwa (as) walimtelekeza na kamwe hakuweza kukutana nao. Hazrat Amma Jaan (ra) anasimulia kwamba upinzani ulikuwa mkubwa sana kiasi hiki kwamba kulikuwa na mwanamke mzee katika upande wa mama wa Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alikuwa analia kwa sababu hakuna hata mmoja anayeturuhusu hata kumuona mtoto Chiragh Bibi. Masihi Aliyeahidiwa (as) alitengwa kama majambazi wanavyofanyiwa kwa sababu alikuwa anaonekana aibu kwa familia. Katika zama hizo, kutegemea kwamba 'Tayee' angeweza kuikubali Ahmadiyya ilikuwa ni kutegemea kitu kisichowezekana na si cha kweli. Mioyo ya watu inaweza kubadilika lakini tunahitaji kuliangalia suala lenyewe.

Masihi Aliyeahidiwa (as) aliupokea utabiri huu wa 'Tayee Ayee' katika muda ule maalum. Utabiri pia ulionyesha kwamba ataingia Jamaat katika wakati ambapo uhusiano wake kwa mtu atakayechukua baiat utakuwa wa 'Tayee' au shangazi. Kama itambidi kuipokea Ahmadiyya wakati wa Masihi Aliyeahidiwa (as) basi utabiri ungekuwa wa maneno tofauti ya 'Bhawaj Ayee' (shemeji amekuja). Kama ingembidi aipokee Ahmadiyya kwa mikono ya Khalifatul Masih I (ra) basi utabiri ungekuwa na maneno kama 'Mwanamke kutoka familia ya Masihi Aliyeahidiwa amekuja' lakini neno maalum 'Tayee' linaashiria kwamba ataipokea Ahmadiyya katika mikono ya mtoto wa kiume wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Kama kusingekuwa na mtoto yeyote wa kiume wa Masihi Aliyeahidiwa ambaye angekuwa Khalifa basi neno 'Tayee' lingekuwa halina maana. Utabiri huu kwa hakika una mambo matatu. 1) Mtoto wa kiume wa Masihi Aliyeahidiwa atakuja kuwa Khalifa. 2)Ataingia Jamaat wakati ambapo mtoto wa kiume wa Masihi Aliyeahidiwa ni Khalifa na uhusiano wake na yeye utakuwa wa shangazi na 3) atakuwa hai kwa muda mrefu. Hii ni kwa sababu wakati Masihi Aliyeahidwa alipoupokea utabiri huu, alikuwa na miaka 70 na utabiri ulikuwa kumhusu mtu ambaye alikuwa mkubwa kwake. Ni jambo kubwa kuwa na umri mkubwa kiasi hicho kwa sababu ubongo wa binadamu hauwezi hata kutabiri hilo kwa mtu kijana kwamba atakuwa hai kwa muda mrefu. Tayee alifariki katika mwaka 1927.

Kwa hiyo, ilikuwa ni ishara kubwa sana kuthibitisha ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa (as) na utabiri huu una ishara nyingi zilizojificha ndani yake. Baada ya kuikubali Ahmadiyyat, 'Tayee' pia alifanya 'Wasiyyat'.

Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba kwa kuangalia aina ya tamaduni na hisia zilizopatikana miongoni mwa watu wa familia za fasheni za kizamani kwa hakika ni badiliko kubwa kwamba aliamua kufanya Wassiyyat. Kwanza kabisa alipinga kwamba kwa nini Masihi Aliyeahidiwa (as) azikwe kwenye makaburi ya familia na kwamba azikwe katika sehemu nyingine. Lakini baadae alifanya Wasiyyat na alizikwa kwenye 'Bahishti Maqbara'. Kwa mtu mwenye busara ni ishara yenye umuhimu mkubwa. Inaweza kuonekana kuwa ni kitu kidogo lakini ina ishara nyingi za ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa (as).

Hazrat Musleh Maud (ra) alipokuwa akielezea tukio la safari ya Masihi Aliyeahidiwa kuelekea Delhi anasema kwamba mtu anaweka tegemeo lake kwa Allah kamwe hawezi kufikiri kwamba kazi zinazofanywa na Allah hazitakuwa na matokea yaliyojaa matunda. Kama unamtegemea Allah pia utakuwa na imani kwamba Allah Ataleta matukio yaliyojaa matunda katika kazi Zake. Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba wakati huo nilikuwa mvulana mdogo wakati Masihi Aliyeahidiwa (as) aliposafiri kuelekea Delhi. Alisafiri kuelekea kwenye madhabahu ya watakatifu tofauti tofauti na akaomba dua kwa muda mrefu na akasema kwamba nimefanya hivyo kwa sababu sitaki vizazi vyao vinyimwe ukweli wa Maishi Aliyeahidiwa(as) ambaye ametumwa katika zama hizi kwa ajili ya kuwarekebisha. Zaidi ya hayo (Masihi Aliyeahidiwa AS) alisema kwamba bila shaka siku itakuja ambapo Allah Ataiangazia mioyo yao na wataupokea ukweli. Hazrat Musleh Maud (ra) anasema kwamba nilikuwa kivulana kidogo sana wakati haya yanasemwa lakini bado yana athari katika moyo wangu.

Hivyo kama Jamaat ya Delhi inataka kuona matokeo yaliyojaa matunda kwa jitihada zao basi waweke tegemeo lao kwa Allah. Siku itakuja ambapo kitu ambacho Allah Anataka kishinde kitashinda. Alisema yote haya wakati akiwahutubia Jamaat ya Delhi. Kwa hiyo, hata leo ni jukumu la Jamaat ya Delhi kusambaza ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa(as) kwa kutumia busara ya hali ya juu kabisa. MashaaAllah harakati hizi za kueneza ujumbe zimeshika kasi kwa kupitia maonyesho. Lakini kuna upinzani pia kutoka kwa Waislam wengine, hivyo bado kuna haja ya kueneza ujumbe huu kwao. Na jambo la muhimu kupita yote ni 'Dua' na jambo hili linahitaji kutupiwa macho sana.

Kisha Hazrat Musleh Maud (ra) pia alielezea njozi ya Masihi Aliyeahidiwa (as) ambamo aliona kwamba kuna korongo refu sana ambamo kondoo wengi wamelazwa na kila kondoo alikuwa na mchinjaji mwenye kisu mkononi mwake na walikuwa wakiangalia mbinguni kana kwamba wanasubiri amri ya Kimbingu. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba katika wakati ule nilikuwa natembea kuzunguka katika sehemu hii. Niliwasogelea na kuwasomea aya hii ya Kuruani Tukufu inayosema 'Waambie, Mungu wangu Atawajalije, kama hamumuabudu na kutii Amri Zake'

Mara tu niliposema hayo, wachinjaji ambao kwa hakika walikuwa ni malaika walielewa kwamba wamepewa ruhusa na walichinja shingo za kondoo wakisema ' Nyie siyo zaidi ya kondoo walao uchafu'. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba aliitafsiri hii kumaanisha kwamba kutakuwa na ugonjwa mkali sana wa kuambukiza na hakika watu 70,000 walikufa kwa ugonjwa wa kuambukiza wa kipindupindu. Hivyo kama mtu haangalii basi Allah Hamjali na hakuna yeyote anayeweza kuzuia Kazi za Allah.

Anasema kwamba baada ya miaka 300 ya Yesu Kristo (as) Ukristo ulikuzwa. Lakini kama tunatafakari hali zetu itachukua muda mfupi sana kushinda huo wakati Ahmadiyyat itabarikiwa kwa ukuaji mkubwa sana na upanuzi InShaAllah. Awe Mulla yeyote wa Pakistani au kiongozi yeyote wa dini au iwe serikali yeyote kubwa ya kidunia, kwa Allah hawana umuhimu wowote. Hao ni tu kama wale kondoo. Na watu hawa hawawezi kuzuia kukua kwa maendeleo ya Ahmadiyyat. Lakini kwa hili hatuwezi kuwategemea wabashiri wetu pekee kwamba ni jukumu lao kueneza Ahmadiyyat. Kama unataka kuwa ni sehemu ya maendeleo haya na ni lazima tuwe sehemu basi nasi pia tujielekeze kwenye dua. Ni lazima tuongeze ucha Mungu wetu. Ni lazima tuimarishe uhusuiano wetu na Allah. Haya ndio mambo yatakayo komesha upinzani dhidi ya Ahmadiyya na yatatusaidia kuweka hisa zetu katika maendeleo ya dini yetu, In sha Allah. Allah Atubariki tupate hali hiyo, Amiin.

Makatibu wa Tahrik Jadid wa matawi ya Dar wajiwekea mikakati

Kutoka uk. 2

Hassan kisha yakafuata maombi ya kimya yaliyoongozwa na Mzee Fadhili Mshamu na mwisho mkutano ulifungwa saa 2.20 usiku kwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Mwalimu Ali Salehe Hassan. Baada ya hapo ilisaliwa sala ya Magharibi na lsha kwa pamoja.

Wakati wa mkutano Mheshimiwa Naib Raisi wa Mkoa, Bwana Mustafa lmrani, aliwasomea washiriki kwa muhtasari hotuba ya Hazur (atba) ya tarehe 11 Novemba wakati akitangaza mwaka mpya wa Tahrik Jadid katika msikiti wa Baitul Nuur huko Calgary Canada. Naye Katibu Taifa Tahrik Jadid Bwana Amiri Kaluta aliwasomea washiriki kwa muhtasari hotuba ya ljumaa ya Hazur (atba) ya tarehe 6 Januari 2017 aliyoitoa katika msikiti wa Baitul Futuh huko London Uingereza wakati akitangaza mwaka mpya wa Waqfu Jadid. Kwa kuzingatia maelekezo hayo ya Hazur (atba) washiriki walipanga mikakati ifuatayo:-

1. Kuunda Kamati maalum ya mkoa ya Tahrik Jadid iii kufuatilia maelekezo ya Hazur(atba).

llipendekezwa kuwa makatibu wote wa Tahrik Jadid wa matawi wawe ndio kamati hiyo.

2. Kuhakikisha kuwa kila mtu analipa mchango wake wa Tahrik Jadid katika tawi lake, sio kulipia kwingine iii kurahisisha ufuatilaji.
3. Kutunza vizuri kumbukumbu za wanajamati kuanzia ahadi na ulipaji.
4. Kuwakumbusha wanajumuiya kila mwezi kuhusu kiasi walichoahidi na kiasi walichotoa na kiasi kilichobaki.
5. Watu waelimishwe kuhusu yakini na imani. Elimu isisitizwe.
6. Makatibu wawe makini kuangalia ahadi zinazotolewa kama kweli zinalingana na hali ya mtu ya kipato. Asiahidi kikubwa zaidi wala asiahidi kidogo sana.
7. Kuwasisitiza watu kutoa michango ya Tahrik Jadid kila mwezi na sio kusubiri mwisho wa mwaka ndio kufanya msisitizo.
8. Matumizi ya mitandao kuhusu kupeana taarifa. Kuwe na website ya Mkoa ya Tahrik Jadid.
9. Viongozi wa Mkoa wawatumie makatibu wa Tahrik Jadid katika kufanikisha zoezi zima.
10. Kutofaya uzembe wa a ina yoyote katika suala Ia Tahrik Jadid wala kuto kula Ia au kusinzia kama Hazur (atba) alivyoagiza.
11. Vikao vya Makatibu wa Tahrik Jadid viendelee. Hiki kisiwe cha mwisho.
12. Wanajumuiya wawe wanakumbushwa kwa wema na upole.
13. Wanajumuiya wahimizwe kutoa michango kwanza wakipata pato kabla ya kuanza matumizi mengine.
14. Mali zingine zisizo pesa zinaweza kutolewa kama michango na Makatibu waweke

mikakati ya kuzigeuza mali hizo kuwa peasa. Mfano mayai, mifugo, mazao, vyombo n.k.

15. Kwa wale wanaolipwa mishahara kwenye benki watoe michango yao kupitia makato ya moja kwa moja benki kwenda akaunti ya Jumuiya.

16. Kuwe na mawasilian ya kutosha na wanajumuiya wote katika tawi. Namba za simu

zijulikane.

17. Kuhakikisha Mkuu wa Kaya anakuwa na faili Ia kutunza kumbukumbu za michango.

18. Kuwe na mahusiano mazuri na wanajumuiya.

19. Watu wanaoshindwa kutimiza ahadi zao waendelee kusisitiziwa kutoa ahadi mpya.

20. Wanajumuiya wahimizwe kumaliza ahadi zao kabla ya mwisho wa mwezi mtukufu wa Ramadhani iii majina yao yapelekwe kwa Hazur (atba) kwa maombi maalum.

21. lazima tushindane na nchi zilizo mbele yetu katika Afrika.

22. Jitihada ifanyike kuhakikisha kuwa idadi ya washiriki katika mchango wa Tahrik jadid inaongezeka kila mwaka.

23. Matawi kumi yanayoongoza katika Tahrik Jadid yawe yanatangazwa.



Makatibu wa Tahrik jadid wa matawi ya Mkoa wa Dar es Salaam wakiwa kwenye picha ya pamoja na Katibu wa Tahrik jadid Taifa bw. Amiri Abedi kaluta mara baada ya kumalizika kwa kikao chao cha pamoja.

Rambirambi kwa kifo cha Sheikh Salehe Mbaruku

Na Sheikh Jamil Rahman

Rabwah Pakistan

Imeniwasilia habari ya kusikitisha sana ya kwamba, ndugu yetu, Sheikh Swaleh Mbaruku wa Duthumi, ametuaga. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

Marehemu Sheikh alikuwa mshupavu mno katika kuhubiri. Niliona kwamba, yeye na mahubiri walikuwa ni kama chanda na pete. Alikuwa na mbinu zake za pekee za kuwafikishia ujumbe wasiojua habari za Jumuiya. Nafikiri Warufiji wanajua sana habari hii. Alikuwa msomi mzuri. Akapenda kujipatia magazeti na vitabu vya Jumuiya na kuvitalii barabbara. Muda niliokuwa Tanzania, aliwahi kunijia Mwamerika mmoja, Earl Martin, aliyenuia kuandika makala maalum kuhusu Jumuiya Ahmadiyya katika Afrika Mashariki ya kupatia shahada ya Uzamivu (Phd). Akaniuliza maswali mengi, nami nikamjibu vya kutosha. Akaniomba nimwazime nakala zote za Mapenzi ya Mungu tangu lianze. Alitaka kutayarisha mikrofilamu yake huko Chuo cha Dar-es-Salaam. Akaahidi kunipatia miye pia nakala ya mikrofilamu hiyo. Tulikuwa hatuna nakala hizo, lakini nilijua kwamba Sheikh Swaleh Mbaruku anazo. Nikamwambia aniletee hizo, naye akazileta kwa furaha. Yule Mwamerika, sawa na ahadi yake, akarudisha baadaye nakala hizo pamwe na nakala ya mikrofilamu yake. Hiyo mikrafilamu nikaiacha ofisini nilipohamishwa kwenda Kenya. Shabaha ni kueleza kuwa nakala zote za Mapenzi ya Mungu zisizopatikana popote, Sheikh alikuwa nazo.



Sheikh Jamil Rahman Rafiq



Sheikh Saleh Mbaruku

Mwanzoni mwa mwaka 1967, nilipowasili Tanzania kwa mara ya pili nikitokea Pakistan, Maulana Shiekh Muhammad Munawwar alinituma niende Morogoro kuwa Mbashiri wa hapo. Wanajumuiya wachahe walikuwepo huko lakini hawakuwa na Mbashiri. Katika zama hizo walionisaidia sana katika shughuli za Jumuiya ni Marehemu Mzee Chamchuwa, Sheikh Swaleh Mbaruku na Bwana Said Lone. Dakta Tufail Ahmad Dar, Mwenyekiti wa Jumuiya ya hapo naye alisaidiana nami sana.

Marehemu Sheikh aliishi huko Duthumi — ama Duthumi. Niliwahi kuitembelea Jumuiya ya hapo pamwe na mke wangu na watoto. Pengine sasa barabara iendayo Duthumi ni ya lami, kwani siku hizo haikuwa ya lami. Basi likipitia sehemu hiyo ya barabara likafika salama Duthumi, kijiji cha Skeikh Swaleh Mbaruku. Mkutano ulifanyika msikitini, uliohutubiwa na Mwalimu Abdu Imrani Mganda na baadhi wengine; sikumbuki kama Sheikh marehemu pia alihutubia, lakini hawezi kubaki nyuma. Miye vilevile niliongea mkutanoni. Tulilala usiku kijijini katika tembe. Ahali zangu wakajifurahia kuitembelea Duthumi. Mvua pia ilinyesha kidogo. Tuliliweka sanduku la nguo chini ya kitanda, lisije likaloa; nasi tulifurahia matone ya mvua yaliyopenya makuti. Lakini mvua ikakatika katika muda mfupi japo ilikuwa imekuja kwa kishindo.

Huko Morogoro, tulipokabiliana na Padre Bendar, Mkuu wa Kanisa la Sabato, marehemu naye alishughulika sana pamwe na ndugu wengine. Siku hizo hizo nililazimika kuondoka Morogoro kwenda Dar-es-Salaam kushika hatamu ya Jumuiya kwa sababu ya Maulana Sheikh Munawwar kuelekea Pakistan.

Nyuma yangu, huko Morogoro, Shiekh Swalehe na vijana wengine waliendelea kumshughulikia Bwana Bendar. Ndugu zetu walikaribishwa kanisani kuongea juu ya masuala ya dini, lakini kwa masikitiko walitendewa vibaya, hata wakasukumwa pia. Basi katika siku chache tu Mungu akaonyesha ishara. Bwana Bendar ghafula akasikia maumivu makali tumboni — kama nilivyoambiwa — akapelekwa hospitali ya Morogoro, kisha akaletwa Dar-es-Salaam na akafia mezani pa opereshani huko Mhimbili.

Bwana Bendar alitokea Afrika Kusini; alikuwa kijana mwenye afya nzuri. Mimi na yeye tulikuwa rika moja. Wakati huo nilikuwa mwenye umri wa miaka 28, wakati sasa nikiwa mzee wa zaidi ya miaka 80.

Marehemu Sheikh Swaleh Mbaruku alikuwa ananitembelea mara kwa mara, tulikaa pamoja, tukala pamoja, tukaongea kuhusu mambo ya dini. Hae, ametuaga! Allah Amweke pema Peponi. Nawapa jamaa zake na wanajumuiya wote mkono wa tanzia. Aliyemwita ni Mpendwa kuliko wote, ee moyo ujitolee tu kwake.

Bustani ya Washairi

SHEHE AMETANGULIA
Na Mahmood Hamsin
Mubiru (Wamamba)

Kwa jinalo nabutadi
Muumba wetu wadudi
Wa milele na abadi
Uloiumba dunia.

Na kwa kila jambo jema
Bismillahi lazima
Ili kupata rehema
Ameagiza Rasua

Ndiwe wa tangu na tangu
Na ni wewe wetu Mungu
Kwa furaha na machungu
Kwako tunakimbilia

Sifa zote bora bora
Kwako zimetia for a
Tunaziona ishara
Mambo yanavyotokea.

Sifa zimekamilika
Kwako ulotakasika
Ni zako Mola Rabukka
Ni mali zake sikia.

Uwezo wote ni wako
Kwa hakika ni chimbuko
Unapotoa tamko
Jambo hilo hutimia.

Si usiku si mchana
Uwezoo tunaona
Kushindikana hakuna
Ambalo wakusudia.

Kwako kun faya kuni
Inasema Qur'ani
Hayo ni yako Manani
Ya uzito kuzidia.

Kila unachokiona
Cha leo hata cha jana
Umeviumba Rabuka
Sivyo visingetokea.

Vya dhahiri na ghaibu
Vyote ni vyako Wahabu
Muumbaji ya ajabu
Yote yanayotokea.

Rabbi umekamilika
Wahadahu la sharika
Ni wewe ulotukuka
Yailahi ya Jalia.

Kisha zishuke salamu
Muhammad Muungamu
Muongozaji kaumu
Ili tusiache ndia.

Rehema kwa walimwengu
Tulokuwa kwenye pingu
Juu pametanda wingu
Ikanyesha ile mvua.

Akavijaza visima
Kwayo maji ya neema
Akina baba na mama
Vyomboni kujitwalia.

Wakajawa na imani
Na mapenzi ya manani
Hata kule utamboni
Wakaweza jitolea.

Muhammad Muokozi
Ang'arae kama mwezi
Mpenzi wetu azizi
Utumwani katutoa.

Akatupa na ahadi
Ya kutujia Mahadi
Kwa jina la Ahmadi
Vumbi kuja iondoa.

Kwetu kafika Sayidi
Masihi tena Mahadi
Kwetu ni kubwa zawadi
Inayozidi rupia.

Kumpokea lazima
Agizo la Muadhamu
Ujahili utazama
Bila yeye kupokea.

Kwisha kwa utangulizi
Ninalo jambo la wazi
Ametawafu mjuzi
Shekhe wetu wa uluwa.

Msiba umetufika
Katutoka Mubaraka
Shekhe aliheshimika
Watu kuwahubiria.

Mtafutaji elimu
Kwa bidii na kwa hamu
Na mengi kayafahamu
Sababu ya kubukua.

Rafiki yake vitabu
Alivipenda ajabu
Alisoma taratibu
Mambo kuyazingatia.

Kaweka na maktaba
Yenye vitabu si haba
Akisoma kwa ratiba
Vitabu alonunua.

Kiswahili kiarabu
Lugha aliziratibu
Kuzisoma pasi tabu
Kusoma na kuongea.

Katika kwake kusoma
Kawakuta maulama
Walojawa na hekima
Habari kumpatia.

Masihi ameshafika
Ewe kijana pulika
Ni amri ya Rabuka
Masihi kumpokea.

Bila kufanya ajizi
Wala bila pingamizi
Akafanya maamuzi
Kujiunga Jumuia

Kisha kuipata sudi
Nae kafanya juhudi
Aifikishe junudi
Ujumbe wake Nabia.

Muumini wake uturi
Siku zote kuhubiri
Taji lake ubashiri
Watu kuwafikishia.

Mapenzi yake ya d hati
Tena ya kila wakati
Kuwahubiri umati
Ili wapate rejea.

Warejee kwa Manani
Waondoke maasini
Na kushika kwa makini
Maagizo ya Jalia

Mawaidha kwa hekima
Ndio ndia ya neema
Taratibu kwa heshima
Bila bughuda kutia.

Na hiyo yao miungu
Usitukane Warungu
Usijezua vurungu
Wako kukutukania.

Usemayo na vitendo
Sambamba huja uhondo
Na ushindi wa kishondo
Waweza ushuhudia.

Huo ndio mwendo wake
Sheikh asiye makeke
Wala hajui mateke
Hiyo ni yake tabia.

Salehe wa Kapilima
Amefanya mambo mema
Ya kueneza neema
Ujaji wa Masihia.

Kapita kugawa mali
Kauli yake Rasuli
Na mali hasa ya kweli
Ukweli kuupokea.

Kaenda dari ma dari
Kuzieneza habari
Za ufikaji Bashiri
Nabii bila sheria.

Utume bila sheria
Huo unaendelea
Hadi mwisho wa dunia
Nuru kutuangazia.

Kwanza kaenda Rufiji
Huko akawapa maji
Si zani ya mfereji
Ya kiroho nakwambia.

Maneno ya ufunuo
Yaangaza ja kiroho
Yanayopenya uzio
Dhambini kutoingia

Rusende huko Nyipara
Kote akatia fora
Na mafunzo bora bora
Vijana kawapatia.

Darasa alifungua
Elimu kuwapatia



Mtunzi na mtungiwa wakiwa kwenye jamvi moja

Qur'ani walijua
Na hadithi za Rasua.

Mantiki na bayani
Yaliyomo vitabuni
Akawapa kwa yakini
Dini yao kuijua.

Hakuwa nayo haraka
Kuwapa yenye baraka
Kwamba Nabii kafika
Yabidi kumpokea.

Wema na mahali pake
Taratibu si makeke
Ujue wapi uweke
Wema ulokumbatia.

Katu haina baraka
Kufanya kitu haraka
Mambo yataharibika
Subira inavutia.

Hiyo njia alishika
Ndiyo ya kati hakika
Yenye wingi wa baraka
Na kuleta manufaa.

Alisuburi wakati
Mzuri na hasanati
Ili afungue nati
Ukweli kuutongoa.

Bila ya matayarisho
Shambalo la korosho
Mbaya ni wako mwisho
Kwanza ni kupalilia.

Matayarisho muhimu
Na hiyo hasa nidhamu
Katu hutakula tamu
Lino ukipuuzia.

Ukisikia mgeni
Anakujia nyumbani
Unapata umakini
Mambo kuweka sawia.

Huwezi kukurupuka
Mambo yataharibika
Upange bila haraka
Mazuri tajichumia.

Maisha bila mipango
Kwenda mbele ni uongo
Ni sawasawa na jengo
Ramani kujichorea.

Kawaambia namba wani
Ni kushika Qur'ani
Ni maneno ya Manani
Yalonyooka sawia.

Kitabu hakina shaka
Maneno yamenyooka
Tena yamekamilika
Kuwaongoza insia.

Rabbi kakipa ulinzi
Ni kitabu kakienzi
Kitadumu hadi enzi
Atapopenda Jalia

Kimeleta uokovu
Na mapenzi lovulovu
Ni kitabu kina nguvu
Maasi kuyazuia.

Na furaha ya rohoni
Ile ya ndani kwa ndani
Chimbuko ni Qur'ani
Kukufanya kutulia.

Bila ya macho huoni
Husikii asilani
Neno ni masikioni
Hapo waweza sikia.

Kama hiyo ni kanuni
Huwezi ona Manani
Pasina na Qur'ani
Hilo halitotokea.

Kila neno lina shani
Humo kwenye Furqani
Ni lulu zenye thamani
Kila neno nakwambia.

Kitabu kimejigamba
Kama hicho kukiumba
Kusanyikeni miamba
Aya moja kuitoa.

Hamuwezi abadani
Jambo haliwezekani
Basi jua kwa yakini
Ni andiko la Jalia.

Hakuna jama ukweli
Nje ya hino Jamali
Ameeleza Jalali
Hakuna kilopungua.

Hakika kina hekima
Ukijaribu kuzama
Utaipata lazima
Mola Ametuwekea.

Cha pili kushikamana
Maendeleo bayana
Na hiyo ndio safina
Ya kuweza tuokoa.

Tutende aliyotenda
Na Rabbi Atatupenda
Mitihani tutashinda
Shetani kumkimbia

Hakika mfano mwema
Kama twataka uzima
Ama sivyo ni dhahama
Na motoni kuingia

Sheikh akaendelea
Mambo kuyafafanua
Ili wapate kujua
Mambo ya kuwaokoa.

Sunna ni yake matendo
Kaonesha kwa vitendo
Hayo kwetu ni uhondo
Muhimu kuzingatia.

Sunna ni jambo muhimu
Dini yetu Isilamu
Tamu na hata la sumu
Waweza kulitambua.

Yafata masimulizi
Aliyosema Azizi
Mambo kuyaweka wazi
Yale yenye manufaa.

Hadithi yakubalika
Isipovuka mipaka
Aloiweka Rabuka
Kwa sisi sote insia.

Kinyume cha Qur'an
Haifai asilani
Si hadithi ni utani
Vigumu kuipokea.

Kisha kawapa habari
Za Muhammad Bashiri
Ametumwa na Kahari
Kukamilisha sheria

Hatokuja asilani
Wa sheria kusaini
Sheria ni Qur'ani
Iso shaka wala doa.

Kwa kueleza sheria
Huyo ameshatokea
Wala hakuna udhia
Ni tamu kama halua.

Sharti awe mpenzi
Wa Muhammad kuenzi
Kwa kilio na majonzi
Dini aweze tetea.

Ampende kweli kweli
Mapenzi yalo makali
Huo ndio urasuli
Ambao umebakia.

Mapenzi kwa Muhammadi
Hiyo ni kubwa zawadi
Hufurahisha Wadudi
Mengi Atakupatia.

Nabii alo kivuli
Cha Muhammad Rasuli
Hilo ni jambo halali
Linaweza kutokea

Ni Nabii mfuasi
Aloipata nafasi
Kwa mapenzi yenye kasi
Muhammad kumwendea.

Nabii Isa afile
Hawezi dumu milele
Amezikwa nchi ile
Inayoitwa India.

Aliyedumu daima
Pasi dunia kuhama
Na ni huyo Muadhama
Nina hamu kumjua.

"Rabbi uliponifisha"
Kwanini sasa wabisha
Mwenyewe kathibitisha
Rabbi Amemchukua.

Kafariki Muhammadi!
Nani tena ni zaidi?
Yeye aishi abadi?
Kifo kumuepushia?

Na mitume wamepita
Hakuna aliyesita
Wote iliwakamata
Amri yake Jalia.

Kila iliyo nafusi
Inayo yake nafasi
Huonja pasi na wasi
Mauti ametwambia

Kaburi la Kashmiri
Si uficho ni dhahiri
Amesikwa ni hayati
Isa mwanae Maria

Ili kuuziba ufa
Twahitaji Ukhalifa
Hiyo ni kubwa raufu
Ya sisi kuendelea

Ukhalifa ndio nguzo
Ya shughuli mzo mzo
Bila khalifa uozo
Nani wa kutangulia

Lini dini Islamu
Kuipata hitiramu
Pasipokuwa Imamu
Khalifa wake Jalia

Kwa sasa tuna Khalifa
Mfufuo walokufa
Ili waipate sifa
Labeka kuitikia

Watu waliathirika
Hayo aliyotamka
Bayati wakazishika
Na kundini kuingia

Hapo ikazuka shari
Maisha yenye khatari
Ya kuchimbiwa kaburi
Wapate kuwafukia

Wanapotoa salamu
Msiijibu salamu
Makadiani ni sumu
Ukae nao khatua

Na kilimo cha pamoja
Msiwete hao waja
Ni ya nini hiyo haja
Hadi kuwakumbatia

Kuwauzia samaki
Nyote mseme sitaki
Itakuwa sio haki
Wao kuwahudumia

Haifai kuwasika
Jeneza lao kushika
Hilo ni kosa hakika
Vibaya kuwasalia

Kuwaoza makafiri
Hilo chungu ja shubiri
Laondoa zetu khari
Na kuleta mabalaa

Hii ilikuwa vita
Nivute nami navuta
Lakini hawakusika
Mashaka kuvumilia

Rusende pakawa joto
Pigo zaidi ya fito
Kila kona kuna moto
Wa kuweza kubabua

Ni kazi ya Kapilima
Aliyewapa uzima
Kwenye haki kusimama
imani kuitetea

Akawapata vijana
Tena vijana mwanana
Wao wakashikamana
Haki kuishikilia

Ikastawi jamati
Ni Lusende katikati
Wakaja wengi umati
Jamatini kuingia

Ikapata washairi
Watunzi wa tabasuri
Wakaeneza habari
Za dini yake Jalia

Mbungiro Watachoka
Kalamu akaishika
Gazetini akawika
Ujumbe kutuletea

Khamisi bini Wamwera
Beti nyingi alichora
Za kuwafanya imara
Jamaat waloingia

Na watunzi kina mama
Kidete wakasimama
Mariam wetu mama
Beti akatutungia.

Hayo yote ni matunda
Sheikh aliyoyapanda
Wakashiba na kuwanda
Wazawa wa Rufijia.

Kisha kenda Mchotike
Waliko ahali zake
Rijali na wanawake
Habari kawapatia

Ilikuwa patashika
Hadi nguo kuchanika
Wengi walikasirika
Ni nini katuletea?

Vipi tutaacha mila
Za baba waliolala
Tuishike shelabela
Hino alotuletea?

Mipango ilifanyika
Ili apate dhurika
Hata kwa roho kutoka
Hili walidhamiria.

Nusura yake Rabana
Sheikh hapo akatoka
Hijira ikafanyika
Pengine kukimbilia.

Huko kawa muhubiri
Wa dini yake Kahari
Kila siku ni safari
Dini kuilingania.

Pembe zote amefika
Sheikh wetu msifika
Kila sehemu kashuka
Nchi yetu Tanzania.

Katu hakuajiriwa
Mshahara kumegewa
Ndio kwanza amekuwa
Sheikh wa kujitolea.

Mjazie ya Manani
Sheikh awe kivulini
Firdausi peponi
Nae apate tulia.

Ni pepo ya watu wema
Waloshika mwendo mwema
Mjalie ya Karima
Matunda kujichumia.

Katu asiwe baidi
Na Mtume Muhammadi
Nae Masihi Mauudi
Aweze wakumbatia.

Tamati nahitimisha
Utungo kukamilisha
Twamuombea maisha
Yale ya kuendelea.

لا إله إلا الله محمد رسول الله

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

P.O. Box 376, Dar es Salaam. Plot 71, Mahamud Street, Opp. Minaret Mmoja Garden. Tel: 2110472, Fax: 2113011.
www.alislam.org www.ahmadiyya.org Email:ahmadiyyatz@gmail.com





HAZRAT MIRZA GHULAM AHMAD AS
www.alislam.org/books/philosophy-teachings.pdf





2017
1438/1439 AH
1397 HS





UPENDO KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Niliyojifunza katika Ibada ya Hija

Hotuba iliyotolewa na Abdulrahman M. Ame sahib katika Jalsa Salana ya mwaka 2016.

Kutoka Toleo lililopita

Hapo Arafa kama maana ya neno lilivyo ni utambuzi wa kina, mahujaji wanatarajiwa wapate kumtambua au wapate maarifa zaidi juu ya Allah na sifa zake na utukufu wake. Kila hujaji ni lazima afike Arafa angalau kabla ya jua kupinduka vinginevyo hija yake haitokamilika.

Mahujaji hukaa hapo hadi mchana na husali Adhuhuri na Alasiri na kabla ya kusali Magharibi huondoka kueleka *Muzdalifah* – (maana yake ni kuwa karibu zaidi). Ikimaanisha hapa hujaji hutakiwa kuwa karibu zaidi na Allah au kupata maarifa ya kumtambua Allah.

Hapo Muzdalifa pia pana muinuko fulani uitwao Al-Mash'arul-Haram. Ambapo Mtukufu Mtume s.a.w. alichanganya sala yake ya Maghrib na Isha hapo na akatumia usiku wote katika kumkumbuka na kumuomba Allah sana sana na kwa moyo wote kama neno *Mash'arul-Haram* linavyomaanisha kwamba ni fikra takatifu.

Kutoka Muzdalifa siku ya mwezi 10 Dhulhija mahujaji baada ya kusali alfajiri au hata kabla huelekea tena Mina. Inasimuliwa kwamba hapo Mina ndipo nabii Ibrahim alipojaribiwa mara 3 na shetani ili kwamba asimtoe mtoto wake dhabihu kwa ajili ya Allah, lakini shetani akashindwa. Basi hapo pana nguzo 3 ambazo mahujaji hutupa vijiwe kwa idadi maalum kama ishara ya kumfukuza / kumpinga shetani. Nguzo hizo *Jamrah Ula*, *Jamrah Wusta*, *Jamrah 'Aqabah*, (ya kwanza, ya kati na kubwa) zinamaanisha kwamba kwa kadri mtu anavyomshinda shetani kwenye hatua za kumwendea Mungu, shetani naye huongeza juhudi zake, lakini mtu hatakiwi kukata tamaa kwani mwisho shetani hurudi nyuma na mtu hupata ushindi.

Kwenye siku hiyo ya 10th *Dhul Hijjah*, baada ya kurusha vijiwe kwenye *Jamrah 'Aqabah mahujaji* ***huchinja wanyama wao wa dhabihu. Kama nafasi inaruhusu Mahujaji hutakiwa kwenda Kaaba kwa ajili ya tawaful Ifaadha (Tawafu ya Nguzo) pamoja na Kusai*** na baadae wananyoa na kufanya mambo mengine waliyokatazwa kabla isipokuwa makutano ya kijinsia, huoga na kuvaa nguo zao za kawaida.

Iwapo hali hairuhusu kwenda Kaaba kwa ajili ya Tawafu ya Nguzo, mahujaji wanaruhusiwa kunyoa na kuvua Ihramu zao mara baada ya dhabihu, na baadae wanakwenda Kaaba kwa ajili ya tawafu ya Nguzo wakiwa na nguo zao za Kawaida baada ya kukaa siku mbili au tatu hapo Minaa kwa ajili ya Ibada ya kupiga vijiwe.

Hatima ya yote mahujaji huzuru tena Kaaba kwa ajili ya tawaful widaa, yaani tawafu ya kuaga.

Hapo kimsingi hija inakuwa imeisha, wengine hutembelea Madina na wanaotaka kubaki Minaa wanaweza kufanya hivyo hadi 12 Dhulhijaa.

Kwa ujumla ibada nzima ya Hija ni kumkumbuka, kumtukuza na kumuomba Allah na hivyo kumbukumbu ya matendo ya kujitolea kwa Allah yaliyofanywa na Hadhrat Ibrahimu na ahali zake yametumika kama kichocheo cha kufikia malengo hayo.



Msikiti wa Makka (Masjidul Haraam) ukionekana kwa upana wake kutokea juu.

Sawa na kauli ya Mtukufu Mtume s.a.w. hujaji anayefanya haya yote kwa moyo wote kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah madhambi yake yote husamehewa, hupata ukaribu wa Allah, kwa maana nyingine hufikia lengo la kuumbwa kwake. Anakuwa mtu mwema, mtawa, asiyeleta madhara kwa viumbe wa Allah, mpole na mwenye msaada na manufaa makubwa kwa ubinadamu.

YALE NILIYOJIFUNZA KWA JUMLA

Kwa upande wa Serikali ya Saudia, imejitahidi vya kutosha kuboresha mazingira ya Hija. Allah Awabariki na Awasaidie zaidi.

Ingawaje zipo pia changamoto za kiutendaji kama inavyoweza kufikiriwa mkusanyiko wa watu zaidi ya milioni 3, si jambo dogo.

Kwa upande mwingine changamoto zinatokana na mahujaji wenyewe ambao wanatokea mazingira tofauti, wakiwa na uelewa na malengo tofauti.

Hivyo kama mtu anakwenda kuhiji akijielewa anakwenda kufanya nini, ibada ya Hija kwake itakuwa na maana kwa sababu Ishara zote zilizotajwa na Allah kama alama Zake, atazishuhudia. Hali kame ya mji wa Makka, Kaaba, kisima cha Zamzam, n.k. pamoja na mkusanyiko wa watu wengi kunadhihirisha uwepo wa Allah na kwamba amri hii hasa inatoka Kwake, kwani mazingira hayo yasiyo rafiki yasingeweza kutembelewa na watu wengi kiasi hicho kama si kwa matakwa Yake Mungu.

Hata hivyo kwa upande mwingine kwa kuziangalia hali za Waislamu tu mtu anaweza hata kukata tamaa na ibada hii, kwa sababu kwa sura ya nje, yale malengo ya Hija yanaonekana yako mbali kufikiwa. Mfano hata katika tukio hili la hija inaonekana bayana kwamba hakuna umoja miongoni mwa Waislam.

- Ingawaje yupo Imam anayesalisha msikiti wa Makka lakini kwa ujumla kunaonekana ombwe la uongozi na mgawanyiko, kwani ukimaliza tu mzunguko wa Haram kuna misikiti inayoonekana kuwa ni ya madhehebu tofauti.
- Ni shida kuweza kuyaona mapenzi na udugu wa kweli wa Kiislamu. Kwa mfano ni jambo nililolishuhudia kwamba unaweza kumsalimia mtu na asijali kukuitikia. Mtu anaweza kukuona upo mbele yake lakini akatema makohozi au kupuliza moshi wa sigara bila kujali kwamba hayo ni maudhi. Watu wanagombea chakula kinachogawiwa kama sadaka. n.k.

Kwa ujumla kinachoonekana ni kana kwamba kila mtu ana lengo lake, wengi wakiwa wamezama kwenye kuitumia hija kwa malengo ya kidunia au biashara. Ingawaje ni kweli biashara haijakatazwa lakini inapopewa kipaumbele kuliko hata matendo yenyewe ya hija, hapo inakuwa si sawa.

- Kwa kushindwa kuelewa falsafa ya Hija, mahujaji wengi wanaonekana kufanya matendo yanayoweza kupelekea kwenye shirki badala ya kukuza Umoja wa Allah ambalo ndilo lengo kuu la Hija. Mfano kwenye kutufu na kwenye kuzuru kaburi la Mtume s.a.w. Madina, kuna baadhi ya watu wanaojisugua kwenye kuta za Kaaba au mlango wa kuingilia chumba cha kaburi la Mtume s.a.w. pamoja na kufanya mambo mengine kwa namna inayoonesha 'mapenzi yasiyozingatia tawhidi.'

MFANANO WA HIJA NA JALSA

Kuna tuhuma kwamba sisi Waahmadiyya hatuhiji Makka badala yake eti Jalsa kwetu ndio Hija.

Tuhuma hiyo si ya kweli, lakini Wanajumuiya tunatakiwa tuijibu tuhuma hii sio kwa maneno tu bali kwa matendo, kwa maana ya kwenda kuhiji kwa wale tulio na uwezo. Sisi Waahmadiyya kwa fadhili za Allah tunayo nafasi kubwa ya kufikia malengo ya Hija kuliko watu wengine kwa sababu tumepewa mwanga wa kutosha wa kuielewa ibada ya hiyo na falsafa zake kupitia mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Kwa mfano Hadhrat Khalifatul Masih III r.a. kuanzia tarehe 31/3/1967 hadi 16/06/1967 alitoa hotuba za Ijumaa ambazo ndani mwake alielezea malengo 23 ya kujengwa kwa nyumba hii ya Allah Kaaba - bila shaka kuonesha upana wa somo hili.



Msikiti wa Madin (Masjidun Nabiyy) ukionekana kwa upana wake kutokea juu.

Masihi Aliyeahidiwa mwenyewe amesema katika moja ya ufunuo alioupata kutoka kwa Allah:

"Yeyote atakayetambua kwamba msingi wa Kaaba uliwekwa kwa hekima ya Mungu huyo ni mwenye hakima, kwa sababu huyo anayo njia ya kutambua maajabu ya ulimwengu.

Moja ya masharti ya kwenda kuhiji ni kwa: "*Mwenye Kuweza*" Na hii ina maana ya uwezo wa mali, afya pamoja na usalama.

Hivyo Mwanzilishi Mtukufu wa Jamaat Ahmadiyya pamoja na sababu zingine zinazoweza kuwepo ambazo zilimzuia asiweze kwenda kuhiji binafsi (kama vile afya yake) lakini pia suala la usalama wake lilikuwa tete. Hasa baada ya yeye kutangaza ujumbe wake, masheikh wa wakati wake walitangaza fatwa ya ukafiri dhidi yake na kwamba anastahili kuuwawa, na hata huko India wako wengi waliojaribu kumuuwa kila nafasi ilipopatikana kiasi hiki kwamba baadhi ya safari ilibidi kupata ulinzi au kutembea kwa hadhari. Hivyo asingeweza kusafiri kwa amani hadi Makka, lakini sawa na njia nyingine ya kufanya hijja - *Hajj-e-Badal* - inayoruhusiwa kisheria, Hadhrat Hafiz Ahmadullah alifanya hija kwa niaba ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Pamoja na kwamba Jalsa haisimami mahala pa hija, hata hivyo kuna mahusiano maalum kati ya Hija na Jalsa.

Maneno yaliyotumika kutoka kwa Allah katika kuamuru Hija kwa Nabii Ibrahim a.s. na Mtukufu Mtume s.a.w. ndiyo hayo hayo yaliyotumika katika kuamrishwa Jalsa kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

"Na Uwatangazie watu habari za Hajj, watakufikia kwa miguu na juu ya kila mnyama mkondefu, wakija kutoka kila njia ya mbali" (22:28).

Maneno haya: "***wakija kutoka kila njia ya mbali***" yametumika pia kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuihusu Jalsa salana.

Kwa hakika bishara hizi zote zinatimia. Kama vile zinavyotimia katika Hija, zinatimia pia katika Jalsa.

Hii pia inadhirisha kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameletwa ili kuondoa yale mapungufu yanayoonekana leo kwa wale wanaoihudumia hija na mahujaji wenyewe - hasa ukosefu wa umoja, udugu wa mapenzi, nidhamu ya uongozi n.k.

Hali ya mazingira ya Jalsa kwa leo yanavutia zaidi upande wa kiroho kuliko vile ionekanavyo kwenye hija kupitia matendo ya Waislamu.

Hivyo kuna haja kubwa ya sisi Waahmadiyya kujilinda na tuhuma zinazoweza kuletwa kupitia Jalsa iwapo hatutozingatia lengo la kuanzishwa kwake.

Ni lazima tuje kwenye Jalsa tukiwa na dhamira ndani yetu ya kufikia malengo ya Jalsa tu na sio vinginevyo.

Tujitahidi kuyafikia malengo hayo, na mtu ajione Jalsa kwake haikukamilika iwapo hakufikia malengo yaliyotajwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. juu ya Jalsa.

Allah Atusaidie sana. Amin.

Ahmadiyya yabisha hodi Mkoani Mwanza

Na Mahmood Hamsin Mubiru – Dar es salaam.

Sheikh Inayatullah Ahmad kabla ya kujiunga na jeshi la Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alikuwa katika jeshi la Malkia wa Uingereza. Huko alijifunza nidhamu, ukakamavu, kufanya kazi bila kuchoka na kutembea kwa miguu masafa marefu. Sifa hizi muhimu kwa muhubiri alikuja nazo alipokubaliwa kuwa Mbashiri a Dini ya Islam na Khalifatul Masih –II Hadharat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra).

Furaha ya Sheikh Inayatullah Ahmad sawa na wale waliofanya kazi naye ilikuwa siku zote kuwaendea watu walipo; mashambani, mijini, mashuleni, viwandani na maofisini na huko kote alifikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Toka mwaka 1948 Sheikh Inayatullah Ahmad alizunguuka Afrika Mashariki akihubiri. Miaka ya 50 na 60 alikuwa Tanzania na alifanikiwa kutembelea sehemu nyingi za Taifa hili. Moja katika safari zake alifika mjini Mwanza. Na kama ilivyo desturi yake alitembelea Ofisi, viwanda, mashule, mashamba n.k akieleza ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Mjini Mwanza alikutana na Wanasiasa ambao tayari alikuwa amekutana nao sehemu zingine za Tanzania. Wepesi wake wa kuchanganyika na watu, bashasha, kulimfanya asipate tabu popote alikokwenda. Kwani viongozi wengi wa nchi hii walikuwa ni marafiki zake. Alijuana na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rashidi Mfaume Kawawa, Abdallah Saidi Fundikira, Haruna Rugusha, Chifu Kidaha Makwaia, Maqaidi na wengineo wengi.

Alipofika Mwanza mwaka 1960 mwaka mmoja kabla ya uhuru wa Tananyika aligawa magazeti ya Mapenzi ya Mungu na kuuza vitabu vingi. Ingawaje hakuanzisha kituo lakini athari za Jumuiyya ziliendelea kutikisa Mwanza kutokana na magazeti na vitabu. Kutoka Mwanza Sheikh Inayatullah Ahmad alikwenda mkoani Mara ambako alifanikiwa kuanzisha Jamaat pale Nyamuswa – Ikizu ambako walipatikana Wanajamaat imara akina Hemed Neema, Rashidi Sumwe na Abdallah Sindoma. Hemed Neema alifanya kazi kubwa ya mahubiri na kwa sababu alikuwa na mahusiano na Mwalimu Nyerere kila alipofika Dar es salaam alibeba vitabu vya Jumuiyya kumpelekea Mwalimu Nyerere nyumbani kwake Msasani. Itakumbukwa ya kwamba Hemed Neema alikuwa mtetezi mkuu wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika ile kesi iliyomkabili Mwalimu Nyerere mwaka 1958 aliposhutumiwa kuwatukana Ma-DC.

Wakati Sheikh Muhammad Munawwar ni Mbashiri Mkuu wa Tanzania alimtuma mwaka 1966 Sheikh Hafidh Muhammad Suleiman kuwa Mbashiri wa Kwanza wa Mkoa wa Mwanza. Hafidh Muhammad Suleiman alipata bahati kujua Kurani Tukufu kwa moyo tangu utoto wake. Alijiunga na Jumuiyya mwaka 1949 na kuhitimu elimu ya Sarf Nahau, Fiqh na Mantiq na baadae alipata Shahada ya H.A (Honours in Arabic) na Shahada ya SHAHID. Baadae alitoa maisha yake yote kuitumikia Jumuiyya ya Ahmadiyya. Tarehe 20 Marchi 1959 aliwasili mjini Mombasa nchini Kenya kutoka Pakistani kwa meli ya SS –Kampala. Alifanya kazi Mombasa, Kisumu na baadae aliletwa nchini Tanzania ambapo Mbashiri mkuu alimpangia Mwanza na Bukoba. Akiwa Mwanza alifanya kazi kubwa ya kueneza mafundisho ya Islam. Alipendwa na kuheshimiwa sana hususan kwa upole wake. Alikuwa ni Mbashiri wa mwanzo huko Mwanza kujiwekea utaratibu wa kuwatembelea wafungwa gerezani.

Mwaka 1968 aliletwa Mwalimu Abdallah Ng'ambage ambaye alikuwa Mbashiri mjini Tanga na huko alifanya urafiki na yule Mshairi Maarufu Sheikh Shaaban Robert hadi kufikia hatua ya watu wa Tanga kumuhesabu Sheikh Shaaban Robert kuwa ni Ahmadiyya. Kwa bashasha zake na uchangamfu Mwalimu Ng'ambage alifanya mahubiri yashike kasi sana mjini Mwanza. Aliamsha mapenzi makubwa kwa Jamaat hususan kwa uhodari wake wa kueneza magazeti. Kwa kutumia umahiri wake wa kutunga mashairi aliwakusanya Washairi na Mwanza ukawa mji wa Washairi. Walikuwepo Mwalimu Khalfan, Bw. Iddi Juma Maganga (Joka kuu) na katika harakati hizo akampata Mwanajeshi Ahmad Ray Makanda ambaye alijiunga na Jumuiyya na kuleta msisimko mkubwa. Bwana Ray alipojiunga na Ahmadiyya hakuficha furaha yake bali aliimba;

Taa inajiwakia, kiza kujikimbilia
Imekuwa kama jua, limulikapo dunia
Naiona kila njia, wapi kwa kuelekea

Vuguvugu hilo la kutumia ushairi kueneza ukweli wa Jumuiyya lilitumiwa vizuri na Bw. Iddi Juma Maganga (Joka kuu) ambaye Oktoba 1967 katika gazeti letu la Mapenzi ya Mungu aliimba;

Wakristo na Sunni, wenye imani hafifu,
Chekeni au lieni, hadi mvimbe mapafu,
Katu haji duniani, Issa aliyetawafu
Lieni kiomboleza, Issa haji duniani.

Itakumbukwa kwamba Bw. Iddi Juma Maganga (Joka kuu) aliwahi kuchaguliwa kuwa Mshairi bora katika miaka ya 1980.

Vuguvugu la Jumuiyya liliendelea na Mwalimu Ng'ambage alipopewa uhamisho akabaki Mwanajumuiyya aliyekuwa Mwalimu Mjini Mwanza Bw. Mukhtari Ahmad Ayyaz. Bw. Ayyaz ana historia ndefu ya kuitumikia Ahmadiyya katika Afrika Mashariki. Ikumbukwe kwamba yeye ndiye aliyeanzisha shule ya BASHIRI HIGH SCHOOL huko Kampala – Uganda ambayo kwa hivi sasa inajulikana kama Ahmadiyya High School. Kwa miaka alikuwa Katibu wa Ahmadiyya mjini Tanga. Akiwa Mjini Tanga Bw. Mukhtari Ahmad Ayyaz alimuhimiza Bw. Ally Sachak wa Tanga kutoa msaada wa mali kuchapisha Kurani Tukufu iliyotafsiriwa na Sheikh Mubarak Ahmad katika lugha ya Kiswahili. Bw. Sachak aliendelea kutoa fedha hadi kufikia zaidi ya Shilingi laki moja. Na Kurani Tukufu ilipochapishwa mwaka 1953 Bw. Ayyaz akiongozana na Sheikh Jalaludin Qamar walimkabidhi Sultani wa Zanzibar wa wakati huo Sultani Khalifa bin Kharoub tafsiri ya Kurani Tukufu katika lugha ya Kiswahili. Sultani Khalifa bin Kharoub alitoa shukrani kubwa sana na akasifu kazi nzuri inayofanywa na Jumuiyya ya Ahmadiyya katika kueneza nuru ya Islam.

Mwaka 1958 wakati wa uchaguzi wa kura tatu, Bw. Ayyaz akiungwa mkono na TANU (Tanganyika African National Union) aligombea Ubunge mjini Tanga. Huko Mwanza Bw. Ayyaz alieneza vitabu na katika shule alizofundisha aliacha athari kubwa. Amezikwa katika makaburi ya Jamaat Ahmadiyya Wailes – Temeke.

Mwaka 1975 Sheikh Yusuf Kambaulaya akitokea mjini Tanga alianza kutumikia mikoa miwili ya Mwanza na Kagera. Mungu bariki katika miaka hiyo ya 70 Wanajamaat wengi walipatikana kwa kuja Mwanza kikazi. Na kama ilivyo desturi ya Wanajamaat wakifika mahala wanakusanyika na kuanza mahubiri. Waliofika Mwanza mwaka 1970 ni pamoja na Bw. Mbwana Mgunda – mwanajumuiyya shupavu aliyeanzisha kiwanda cha Kengele za Baiskeli na kuwaajiri Wanajamaat. Pia alijitolea pesa ili gazeti la Mapenzi ya Mungu liendelee kuchapishwa.

Mwalimu Ramadhani Khalfan alikuwa Mwalimu maarufu wa Kiswahili katika shule ya Lake Sec, School. Abdulrahman Nyamihasi, Dr. Iddi Mwanga – Daktari mashuhuri aliyekuwa hospitali ya Muhimbili na akiwashangaza watu waliokuwa wanamfahamu walipomuona na kapo la vitabu huko Kariakoo akiuza vitabu vya Dini na walipokuwa wanamuuliza vipi? Muhimbili natibu maradhi ya mwili, hapa natibu maradhi ya kiroho. Mussa Nyengo aliyekuwa anafanya kazi Tanzania Elimu Supply na Bw. Kassim Mrisho Maftah aliyekuwa anafanya kazi Lint and Seed marketing Board. Mahali pa kusalia palikuwa hapatoshi na hivyo fikra zao, mazungumzo yao na usumbufu wao ilikuwa ni namna ya kupata pahala pa kusalia. Wanajumuiyya hao waliendelea na maombi na kufunga saumu. Allah alipokea maombi yao na mwaka 1976 Mwalimu Ramadhani Khalfan alifanikiwa kupata kiwanja kizuri tena katikati ya jiji la Mwanza. Kiwanja kipo mtaa wa Rufiji na Unguja. Kwa haraka, ushujaa na jazba kubwa Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya alikishughulikia kiwanja hicho na hatimaye Jumuiyya ya Ahmadiyya kukimiliki kwa halali. Matukio ya baadae hata hivyo ni ya kusikitisha kwani kama tutakavyoona kuwa kiwanja hicho kilivamiwa. Kuna haja hasa ya kueleza kwa ufupi mgogoro wa kiwanja hicho Msikiti.

Mwaka 1970 baada ya mahangaiko makubwa, Jamaat ya Mwanza ilifanikiwa kupata kiwanja cha kujenga Msikiti kama tulivyotangulia kusema hapo juu kiwanja hicho kipo mitaa ya Rufiji na Unguja. Kiwanja hiki kilivamiwa na kundi la Waislam na kujenga shule iliyoitwa jina la SAKAFA HIGH SCHOOL. Jamaat ya Mwanza ilipeleka malalamiko Mahakamani. Kwa ushujaa na h ekima kubwa kesi ilisimamiwa na Sheikh Ahmad Daud Mmoto akishirikiana na Wanajamaat wafuatao:- Bw. Idrisa Sengoga, Mwalimu Omari Matimbwa, Bw. Ismail Doto, Bw. Juma Ngayapula, Mzee Salum Thani na Mzee Saidi Bakari Sasamka. Kwa msaada mkubwa wa Allah Jamaat ilishinda na Mahakama ikaamua kuvunjwa majengo yao. Hata hivyo Makao Makuu ya Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Dar es salaam yalitoa rai kuwa badala ya kuvunjwa wapatiwe kiwanja mbadala. Kimsingi wenye shule walikubali rai hiyo lakini miaka mitano ilipita bila jambo lolote kufanyika. Kesi ikaenda tena mahakamani safari hii kesi ilisimamiwa na Bw. Ahmad thani, Yahya Kambaulaya na Yusuf Kachima. Kwa msaada mkubwa wa Allah Jumuiyya ya Ahmadiyya kwa mara nyingine ikashinda. Mgogoro huo wa kiwanja cha Msikiti Mwanza ndivyo ulivyo kwa hivi sasa.

Wakati tunazungumzia mgogoro huu inatubidi kuwakumbuka Wabashiri waliofanya kazi kubwa Mjini Mwanza. Na hao ni pamoja na Sheikh Hafidhi Muhammad Suleiman, Mwalimu Abdallah Ng'ambage, Sheikhi Yusuf Athumani Kambaulaya, Mwalimu Saidi Mgeleka, Sheikh Ahmad Daud Mmoto, Sheikh Abutalib Iddi Sandi, Mwalimu Mubarak Nyamihasi, Mwalimu Ramadhani Mahmood, Mwalimu Yusuf Gesonko na Sheikh Waseem Ahmad Khan.

Kwa miongo mitatu Jamaat ya Ahmadiyya mjini Mwanza imekuwa ikikabiliana na kukosekana kwa mahala pa kusalia. Ufumbuzi uliojitokeza ulikuwa ni wa muda na si wa kudumu. Kwa mathalani Dr. Iddi Mwanga alipokuwa hospitali ya Bugando sala ya Jamaat ilikuwa inafanyika nyumbani kwake. Na alipoondoka sala ilikuwa inafanyika kule Nyamanoro alikokuwa anaishi Mwalimu Saidi Mgeleka. Hata hivyo vitimbi vilifanyika na wakazuiwa kusali Jamaa. Kutoka hapo ilionekana ya kwamba ni vizuri kwenda kusali katika nyumba za Wanajamaat. Kwa mfano walikwenda kusali kwa Bw. Matimbwa na nyumbani kwa Bw. Idrisa Sengoga. Sheikh Daud Mmoto alipohamishiwa Mwanza alipangiwa huko Bugando na hivyo huko pakawa mahala pa kusalia. Kutokana na usumbufu huo wa muda wa mrefu Mzee Thani alitoa sehemu ya kiwanja chake ili ujengwe Msikiti. Na huo ndio Msikiti ambao unatumika kwa hivi sasa. Msikiti huo umetokana na juhudi hiyo ya Mzee Thani. Baaa ya kutolewa eneo hilo Mzee Thani na Bw. Yahya Kambaulaya walishughulika kwa hali na mali katika ujenzi wa Msikiti. Hawakupumzika wala kusinzia hadi Msikiti ulipokamilika. Wanajamaat wa Mwanza kwa ujumla wao walishiriki katika ujenzi wa Msikiti huo.

Mahali hapo ni pazuri na palipo wazi karibu na kituo kikuu cha mabasi. Kwa hakika ni Msikiti ambao unatoa faraja kubwa kwa watu waliokuwa wanatangatanga jangwani kwa miaka twende miaka rudi.

Mwaka 2015 aliwasili Mjini Mwanza Sheikh Waseem Ahmad Khan ili kushughulika na ujenzi wa Msikiti mkubwa wa Mkoa. Kiwanja kile kilichotolewa na Mzee Thani na Bw. Yahya Kambaulaya kilibadilishwa matumizi yake katika vyombo vinavyohusika na kiwanja hicho kikakubaliwa kuwa kiwe cha ujenzi wa Msikiti. Kazi hii wakati nikitembelea Mwanza mwezi July, 2016 nyumba ya Mbashiri ilikuwa tayari na m ipango ilikuwa mbioni ya ujenzi wa Msikiti.

Jamaat ya Mwanza ni mfano unaong'aa kwa Wanajamaat ambao wako tayari kujitolea kwa hali na mali. Kujitolea kiwanja cha Msikiti ni ishara ya watu wanaotanguliza dini mbele ya dunia. Mapokezi niliyoyapata mimi ndugu yao wa kiroho hayawezi kufutika moyoni. Sheikh Waseem, Mwalimu Nyamihasi, Mwalimu Yasini ukweli walinionesha mapenzi makubwa. Msaada mkubwa niliopewa na Bw. Yahya Kambaulaya umeniwezesha kufanya kazi yangu ya utafiti kwa wasaa na utulivu. Allah Amzidishie moyo wa kuipenda na kuithamini Jamaat. Tutaendelea kuzungumzia juu ya yale niliyoyaona Mwanza katika makala zinazofuata. Inshallah.

Mahafali ya Kidato cha Nne Ahmadiyya Sekondari Yafana

Kutoka uk. 12

shule alisema kuwa, Tayari shule imeisha jenga Maktaba na Maabara kubwa ili kukidhi haja ya serikali ambayo imetangaza kuwa, kuanzia mwaka kesho (2017) wanafunzi wote watasoma masomo ya sayansi. Changamoto sasa ni kuhakikisha vifaa kwa ajili ya maabara vinapatikana ili kukidhi haja ili kuleta ufanisi katika masomo.

Mwenyekiti wa kamati ya shule Sheikh Abdulrahman Ame akiongezea katika maelezo ya Meneja wa shule alisema, ni kweli yapo maendeleo kadhaa yaliyopatikana hapa tangu tulivyoanza hadi hapa tulipo. Pamoja na hayo ni mpango wa kamati ya shule hapo baadae kuwa shule yetu iwe na kidato cha tano na sita ili kuwaendeleza vijana wetu katika elimu ya kiwango juu Inshallah.

Akitoa nasaha zake kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi , Katibu wa Elimu wa jumuiya ya Waislama wa Ahmadiyya nchini Bw, Badru Musoke aliwakumbusha wahitimu jukumu kubwa lililo mbele yao ni kufanya biashara na Mwenyezi Mungu. Alisema hadi kuona shule hii imefikia hapa, kuna juhudi kubwa zilozofanywa na vijana kama ninyi. Hivyo kuhitimu kwenu kuwe ni mwanzo na chachu ya kuitumikia Jamaati yetu ili mje kuwasaidia ndugu zenu na wadogo zenu kama ambavyo watu walijitolea kwa ajili yenu hadi leo hii nanyi mnahitimu.

Shamra shamra za mahafali haya ziliongezwa nakshi na viburudisho vya aina mbalimbali. Mashairi ya kuwaaga wahatimu vidato mbalimbali yalighaniwa kwa ufundi mkubwa ulio yeyusha nyoyo za wasikilizaji. Bashiruddin shaib mbawala na Twahil Bilal ambao ni wanafunzi wa kidato cha tatu walighani shairi lenye kibwagizo “wacha ibaki stori, kwa form 4 ya tatu”. Wasichana wa kidato cha tatu nao walighani shairi lenye kibwagizo kisemacho “Tuwaombee salama, kumbukeni mambo mema”. Kidato cha kwanza waliwaaga ndugu zao kwa shairi lilosema “ Twawaombea Baraka, wapendwa msibadilike”. Na upande wa wahitimu Bilal Kaluta alighani shairi la kuwaaga waliobaki akisema “Tunawatakia heri, tunawaaga kwa heri” na wasichana Zabib S.kazema na sharifa A.Ng’amilo waliimba wimbo mzuri kwa lugha ya kiingereza kuwaaga wadogo zao.

Kulikuwa pia na vijana wa skauti ambao walitoa burudani nzuri kwa michezo mbalimbali na pia kuonesha umahiri wao upande wa gwaride. Hakika mahafali yalifana kwa kiwango kilicho stahili.

Mgeni wa heshima Amir na Mbashiri mkuu wa Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya Tanzania, sheikh Tahir Mahmood Choudhry kabla ya kutoa nasaha zake alitoa vyeti kwa wahitimu wote. pia alitoa vyeti maalum na kwa mwanafunzi mwenye nidhamu, aliyeongoza kwa usafi, aliyeongoza kwa taaluma katika kipindi chote cha masomo yao.

Mgeni rasmi alianza kuelezea historia fupi ya ujenzi wa shule zinazo endeshwa na Jumuiya. Alisema miaka ya 70 khalifa wa tatu wa Masihi Aliyeahidiwa alianzisha mpango wa Nusrat Jahan (huduma kwa ulimwengu) kwa ajili ya kuwasaidia walimwengu. Katika upande wa Afrika Magharibi huduma hii imeendelea sana kwa kujenga shule nyingi kinyume na Afrika ya Mashariki.

Shule hizi hazikuanzishwa kwa ubaguzi wa aina yoyote, iwe dini au vinginevyo. Hatufanyi biashara katika shule zetu bali tunatoa huduma. Gharama tunazo toza ni kwa ajili ya huduma kwa wanafunzi wenyewe. Maendeleo mengine yote hayafanyiki kutokana na vyanzo vya shule bali kutoka mifuko yetu mingine ya Jamaat.

Akijibu risala kuhusu changamoto zinazo ikabili shule alisema, nimepokea matatizo yaliyo katika risala kama ujenzi wa uzio na upungufu wa makazi ya wanafunzi, Inshallah tutaendelea kutatua changamoto hizo kadri itakavyo wezekana.

Pia aliwapongeza kamati ya shule, mkuu wa shule, meneja na walimu kwa jitihada walizozifanya katika kuisimamia shule.

Alisema shukrani za dhati ni kwa waalimu wote waliotumia muda wao kwa kujitolea kwao. Hakika nawashukuru sana kwani ni kwa ushirikiano wao ndio shule yetu leo imefikia hapa.

Wazazi na wanafunzi ni mashahidi juu ya shule ilivyoanza kwa udhalili sana. Lakini leo Alhamdulillah. Anatambua pia mchango wa wazazi kwa ushirikiano walioutoa katika shule kuwa ni moja ya chachu ya mafanikio yetu.

Aidha aliwashukuru wanafunzi kwa kukaa shuleni kwa nidhamu katika kipindi chote cha masomo yao. Hali hiyo imekuwa ni moja ya jambo linayo ipatia sifa njema shule yetu Alhamdulillah.

Amir Sahib alisema amepokea pongezi kwa mzazi ambaye mtoto wake anasoma shuleni hapa kwa kusema kuwa mwanae amebadilika sana tangu alipotoka shuleni petu. Alhamdulillah.

Mwisho aliwaasa wanafunzi kushikamana na elimu. Kwa sababu elimu ndio inayoweza kutoa tofauti kati ya anayejua na asiyejua. Mtume s.a.w alisema tuitafute elimu hata uchina. Hivyo wanafunzi walio hitimu, leo isiwe mwisho wa masomo yao bali hapa ni kama mwanzo. Wazazi wenye uwezo wasisite kuwaendeleza pale panapo wezekana wao kuendelea na masomo.

Amir Sahib aliiombea shule yetu kwa Allah ipate mabadiliko makubwa ili iwe chachu ya vijana watakao itumikia nchi na Jumuiya yetu.

Baada ya maombi na kufunga shughuli za jukwaani, ulifunguliwa uwanja wa kupiga picha na pia wazazi kuwapongeza wanawao kwa zawadi na mashada, shamra shamra ambazo ni vema kama utabahatika kusikia mahafali mengine uhudhurie ili uwe shuhuda wewe mwenyewe. Mahafali yaliandamana na maakuli,uwanja huu nao huwa ni vigumu kuelezea ladha tamu ya vinywaji na vyakuwa vilivyo andaliwa.

Baada ya mahafali, tunawaombea matokeo mazuri wahitimu hawa ili waweze kuendelea mbele katika masomo. Amin .

Kumbukumbu kwa rafiki yangu anayeteswa kwa ajili ya Imani



Kushoto ni Sheikh Saba Zafar ambaye amekamatwa na polisi nchini Pakistan kwa ‘kosa’ la ‘kufanya kazi kwenye ofisi ya tahrik Jadid’ mjini Rabwah. Kulia ni sheikh Ansar Hussain aliyepo hapa Tanzania (mtumzi wa shairi hili)

Wewe ni rafiki yetu
Waishi moyoni mwetu
E Saba Zafari wetu
Sisi twakupenda sote

Wewe ni habibu wetu
Mkazi wa macho yetu
E Saba Zafari wetu
Tunakukumbuka sote

Ewe mbashiri wetu
Wewe ni fahari yetu
E Saba Zafari wetu
Sisi tunalia sote

Leo wanacheka sana
Polisi wa Pakistana
E Saba Zafari wetu
Ukadhulimiwa sana

Tusubiri na onana
Kesho watalia sana
E Saba Zafari wetu
Mungu Anaona sana

Mzee Yusuf Ngarombe Ametutoka



Mzee Yusuf Ngarombe ameaga dunia tarehe 10 Januari 2017 huko nyumbani kwake Nachingwea, Lindi.

Jambo ambalo hatuwezi katu kusubiri kuwaambia ni kwamba mzee Ngarombe alikuwa ni shujaa na mtetezi wa imani yake. Vitisho vingi alivipata alipompokea Masihi Aliyeahidiwa - Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. lakini kama ilivyo ada kwa wale waliopata *‘ilmul yaqiin’* bw. Ngarombe kwa vitendo alionyesha kuithamini imani yake kuliko kitu kingine chochote kile. Kwa mathalan uamuzi wa kaumua kutoka kilipo kitovu chake sio uamuzi mdogo. Yeye alichukua hatua hiyo na kuwa miongoni mwa Muhajrina wa mwanzo katika Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania.

Habari zaidi kuhusu Mzee Yusuf Ngarombe zitaandikwa kwenye toleo lijalo. Inshallah.

Kumalizika na kuanza kwa mwaka

Kutoka uk. 12

kwa ajili ya kuwoanesha watu. Je matamanio yaliyojificha ndani ya nyoyo zetu yako dhidi ya Allah. Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametupatia maelezo ya kina juu ya hili kwa kusema:

Kutangaza umoja wa Mungu hakufikiwi kwa kutamka tu 'Lailaha ilAllah' lakini mtu akabaki na kundi la masanamu moyoni mwake. Kila mtu anayetoa umuhimu zaidi kwa kazi yake, kwa mipango yake na mbinu zake kuliko ambavyo anatoa kwa Allah au anamtegemea mtu fulani zaidi kuliko anavyomtegemea Allah kwa hitajio lake lolote, au anajitukuza zaidi mwenyewe kwa namna ambayo utukufu huo alitakiwa autoe kwa Allah basi katika hali hizi zote mtu huyo anafanya Shirki. Basi kuna haja ya kuviangalia viwango hivi kwa kina na kisha tujifanyie tathmini

Kisha baada ya hayo kuna haja ya kutafakari iwapo kwamba katika mwaka uliopita tumejilinda na uongo na tumetembea juu ya njia ya ukweli? Kwa mfano, iwapo tulikutana na mazingira ambayo kusema ukweli kungetuweka kwenye kupata hasara za kidunia, je hatukusema uongo. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Kusema ukweli kuna gharama kubwa na ushahidi wake wa kweli ni ule wakati ambapo maisha ya mtu, mali yake na heshima yake vipo hatarini.

Kisha kuna swali jingine, je tumejiepusha na yale mambo ambayo yanaingiza mawazo maovu nyoyoni? Kwa mfano katika dunia ya leo kuna televisheni na intaneti ambazo kuna vipindi vingi sana ambavyo kwa kuviangalia vinapelekea kwenye mawazo machafu, je tulijikinga na kuangalia vipindi hivyo? Iwapo tunaangalia michezo michafu na vipindi ambavyo vinayapeleka mawazo yetu mbali na ahadi tuliyofunga basi hali yetu inatakiwa itutie hofu. Mambo haya humsukuma mtu kwenye 'Zina'

Kisha kuna swali jingine, Je tumejilinda dhidi ya kutazama kusikoruhusiwa na bado tunaendelea kujilinda? Kuhusiana na kuyalinda macho, hii ni amri kwa wanaume na wanawake pia. Wanaume na wanawake wote wanaamriwa kuinamisha macho yao chini na kulinda heshima zao.

Kisha kuna swali jingine, Je tumejilinda dhidi ya migogoro ya kijamii na machafuko? Mtukufu Mtume s.a.w. alisema kutumia maneno ya kuudhi dhidi ya mwaminio ni "Fisq" (Uovu).

Kisha kuna haja ya kujiuliza sisi wenyewe iwapo tumejikinga na aina zote za uonevu. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema kuchukua ardhi ya mtu mwingine hata kwa upana wa kiganja au hata kuchukua sehemu iliyo kama kijiwe kidogo ni kinyume na sheria ni ukatili na ni kumuumiza mwingine. Hivyo hivi ni viwango ambavyo tunatakiwa tujipime sisi wenyewe.

Swali lingine ambalo tunahitaji kujiuliza ni kwamba je tumejizuia dhidi ya vitendo vya usaliti? Mtukufu Mtume s.a.w. alisema Usimfanyie hila hata mtu yule ambaye anakuasi. Hiki ni kiwango kilicho mbele yetu.

Kisha, Je sisi tulijilinda na aina zote za uovu? Mtukufu Mtume s.a.w. alisema kwamba watu waovu kabisa ni wale wasio watii. Kuna watu wanaopenda uwepo mtengano kupitia masengenyo. Wanapenda kusambaza siri za watu na kuwaleza wengine. Watu ambao wanasababisha watu wengine wasielewane hao ni waovu. Watu ambao wanawakwepesha watumishi wema wa dini na Jamaat kutoka kwenye utii hao kwa hakika ndio watu waovu.

Kisha kuna haja ya kujitathmini; Je tumesimamisha sala zetu tano kila siku kwa kudumu kwa mwaka mzima uliopita? Allah ametuamrisha juu ya hilo sehemu kadhaa katika Quran tukufu. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema mtu kuacha sala kunampelekea kwenye ushirikina na ukafiri.

Kisha kuna haja ya kujiuliza, Je tumesali sala za Tahajjud? Mtukufu Mtume s.a.w. alisema jitahidini kusali sala ya tahajjud kwa kudumu kwani hiyo ni njia ya kufikia utawa na wema. Kufanya hivyo kutakusaidia kupata mapenzi ya Allah. Pia kusali tahajjud kunakukinga na kufanya maovu, kunafuta makosa na kunaleta afya ya kimwili pia.

Kisha kuna swali lingine la kujiuliza. Je tumeleta Durood (kumsalia Mtukufu Mtume s.a.w.) kwani hiyo ni moja ya amri za Allah na ni njia ya kuyafanya maombi yetu yakubaliwe. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema iwapo utaomba lolote bila ya kuleta Durood basi ombi hilo linabaki baina ya mbingu na ardhi. Hivyo maombi yenu hayawezi kufika mbele ya Allah iwapo hamkuyapa nguvu kwa Durood.

Pia inabidi tujiulize iwapo tumeendelea kuomba maghofira sana. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema mtu ambaye anaomba maghofira na kutubu kwa Allah kwa kudumu Allah Anamfanyia njia za kuepukana na ugumu katika mambo yake na Anamrahisishia njia zake za kupata riziki kwa namna ambayo mwenyewe hawezi kuwaza kwamba inaweza kutokea hivyo.

Pia kuna haja ya kutafakari iwapo tumeendelea kuzama katika kumkumbuka na kumtukuza Allah. Mtukufu Mtume s.a.w. amesema kazi yoyote ambayo inafanywa bila ya kumtukuza na kumsifu Allah inabaki na upungufu. Inakosa baraka na uzuri ndani yake.

Pia, Je tumebaki na hadharai ya kutokuwaudhi wengine wawe ni jamaa zetu au laa. Je mikono yetu na ndimi zetu zimejizuia kuwaudhi wengine? Je tumewasamehe waliotukosea kwa mwaka uliopita? Je unyenyekevu na upole vimekuwa ni sehemu kubwa ya tabia zetu? Je tumebaki kuwa wanyenyekevu kwa Allah katika nyakati zote za furaha, misiba, ufaulu na umaskini badala ya kuwa watovu wa nidhamu? Iwapo ulimhoji Allah katika matatizo yaliyokufika basi huwezi kuwa mwaminio wa kweli. Je tumejilinda dhidi ya tabia chafu na mila zisizofaa? Mtukufu Mtume s.a.w. alisema mila za namna hiyo na uzushi (bidaa) zinapelekea kwenye upotevu, hivyo jiepusheni nazo.

Je tumejibidiisha kufuata amri za Quran tukufu na mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. ? Je tumejitahidi kujiepusha moja kwa moja au angalau kujaribu kujiepusha na kiburi na kujionyesha? Baada ya shirk kosa kubwa kinalofuata ni kiburi na majivuno. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema mtu mwenye kiburi hawezi kuingia peponi, na kiburi ni pale mtu anapokataa ukweli, anapowadhani wengine kuwa duni na kuwatendea kwa ubaya.

Na je tumejitahidi kufikia viwango vya juu vya tabia njema? Je tumejitahidi kushika unyenyekevu na unyonge? Umuhimu wa kuwa mnyonge unaweza kuonekana katika dua ya Mtukufu Mtume s.a.w. ambayo alikuwa akiomba: O Allah nijaalie niishi miongoni mwa wanyonge, unifishe nikiwa miongoni mwa wanyonge na ukanifufue miongoni mwa wanyonge.

Kisha, je tuliendelea kuomba na kuwakumbusha watoto wetu wawe watiifu kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kuzidi kuboreka kila siku? Je tumefikia kiwango cha kumtii Masihi Aliyeahidiwa a.s. kiasi hiki kwamba mambo mengine yanakuja baadae? Je tumeomba ili tuendelee kubaki kuwa watiifu kwa Ukhalifa? Je wazazi wote wamewaelekeza watoto wao juu ya umuhimu wa Ukhalifa na wamewaongoza ili wabaki kuwa watiifu kwa Ukhalifa, na je tumeomba ili Allah awape mwelekeo huo. Je tumemuombea Khalifa kwa kudumu na tumeiombea Jamaat?

Basi iwapo majibu ya maswali hayo ni Ndiyo, basi pamoja na madhaifu na mapungufu tuliyonayo tutakuwa tumepata faida kwa mwaka uliopita lakini iwapo majibu ya baadhi ya maswali ni Hapana basi hiyo ni hali ya kutisha na inatubidi tutafakari sana juu ya hali zetu.

Allah Atusaidie ili tuweze kuyajenga maisha yetu sawa na mafundisho haya ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Ameen.

Allah Atusaidie kutimiza ahadi zetu tulizofanya na Atujaalie kuutumia umri wetu kwa kupata radhi za Allah na Atujaalie tuweze kuishi sawa na matarajio ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. na Atufanye tuwe mifano mema kwa wengine, Ameen.

Masihi Aliyeahidiwa (AS) alisema: 'Jamaat yangu yote waliopo hapa na wengine wausikilize ushauri huu kwa umakini sana kwamba wale walioingia katika Jamaat hii na wanahusiana nami wakiwa ni wafuasi wangu, inakusudiwa kwamba kwa kufanya hivyo wapate vitendo vyema na wafikie kiwango cha juu kabisa cha Ucha Mungu na utawa na kusiwe na fitina wala matendo mabaya yanayoweza kuwasogelea. Wawe ni watu ambao wanasali Sala tano kwa siku, wanajiepusha na kutokuwa waaminifu, kamwe hawamdhuru yeyote kwa ulimi wao, kamwe hawafanyi jambo lolote la kosa, na wawe wasio na hata wazo la kufanya tendo lolote la madhara, hivyo wanajizuia na vitendo vyote vya jinai, maneno mabaya, vitendo vyenye madhara, na hamasa mbaya na matendo yasiyo ya kiuchaMungu. Na alisema kwamba wawe ni watu wa Allah wenye moyo safi ambao hawaenezi mgogoro wowote na ambao ni wapole, watu wema na wasiwe na aina yoyote ya mawazo mabaya katika roho zao. Ni lazima iwe kanuni yao kuwasaidia binadamu na wawe wenye kumuogopa Allah na wailinde mikono yao na ndimi zao na mioyo dhidi ya utovu wa uchaMungu na ni lazima wasali mara tano kwa siku kwa unyenyekevu wa hali ya juu kabisa na wajilinde dhidi ya kuwatendea watu vibaya, uharamu, rushwa na upendeleo. Wasikae na makundi mabaya. Na kwa hiyo hampaswi mnatakiwa msiwe na uhusiano wowote na mtu ambaye hatimizi Amri za Allah au ambaye hajali kutimiza haki za watu, au ambaye tabia yake ni ya kifitina au ambaye hana uchaMungu katika vitendo vyake au ambaye hana fikara nzuri kuhusu Masihi Aliyeahidiwa (as) na ambaye anawadhuru watu wengine kwa matendo mabaya.

Hivyo jitengeni na kuwa na urafiki wa aina yoyote au uhusiano na mtu ambaye hana heshima kwa Masihi Aliyeahidiwa (as). Lakini hii haina maana kuwa muache kueneza neno la Allah. Jilindeni tu na watu ambao wanamtukana Masihi Aliyeahidiwa (as) na wanaitukana Jamaat na ambao wanakaidi ukweli kwamba Masihi Aliyeahidiwa (AS) ndiye Masihi wa zama.

Masihi Aliyeahidiwa (AS) kisha anasema kwamba kamwe usinuie kumdhuru yeyote kutoka katika dini yoyote au taifa lolote au kabila lolote. Kuwa msaidizi wa kweli kwa kila mtu na kamwe usimruhusu yeyote miongoni mwa aina ile ya watu wenye tabia mbaya waingie kwenye kundi lenu au majumbani kwa sababu kama watakuwa karibu yenu, mtateseka. Haya ni masharti ambayo nimekuwa nikiyarudia tokea mwanzoni. Kila mwanajumuiya katika Jumuiya yangu anatakiwa kuyafuata na mikutano yenu isiwe na uchafu wowote au porojo au dhihaka na tembeeni mkiwa na mioyo safi na mawazo safi. Kumbukeni kwamba kila fitina isijibiwe na jaribuni kuacha baadhi ya hali zijipitie na jifunzeni kusamehe na kuonyesha subira.

Kamwe msifanye shambulio kwa yeyote kwa njia zisizo za halali. Na jaribuni kuzidhibiti jazba zenu. Kama mkiwa katika mabishano au mjadala wa kidini basi fanyeni hivyo kwa upole sana na staha. Kama mtu akiwatendea vibaya au akiwatukana basi semeni tu Salaam na ondekeni katika kikao hicho. Na msiwe wenye matusi au wenye tabia mbaya katika kujibu vinginevyo kutakuwa hakuna tofauti. Allah Anataka kuwafanyeni nyote kuwa ile Jamaat ambayo mnakuwa ni mfano wa uchaMungu na wema kwa kila mtu. Humo muwaondoe watu wote miongoni mwenu ambao ni mfano wa fitina, tabia mbaya na maovu. Mtu ambaye yumo katika Jumuiya yetu asiyeweza kuishi ki kawaida, kiwema, kudumu katika matendo mema, laini katika uzungumzaji na tabia za kiuchaMungu haruhusiwi kuwa miongoni mwetu. Kwa sababu Mungu wetu Hahitaji mtu wa aina hiyo aishi miongoni mwetu. Na mtu huyo bila shaka hatakuwa na Akhera nzuri kwa sababu hakufuata

Hivyo kaeni kwa hadhari na kuweni na moyo mweupe na asili ya upole na mtatambulika kwa kusali kwa wakati na kwa khulka njema. Yeyote mwenye mbegu za maovu zilizo kwenye moyo wake hatoweza kujiunga nasi kwa muda mrefu. Inatakiwa kwamba mioyo yenu iwe haina taka za udanganyifu, mikono yenu ilindwe dhidi ya tendo lolote baya na macho yenu yawe salama dhidi ya uchafu wowote na ndani yenu kusiwe na chochote isipokuwa ucha Mungu na uwezo wa kuhisi mahitaji ya viumbe wa Allah. Ninategemea kutoka kwa marafiki zangu wote wanaoishi pamoja nami hapa Qadian kwamba watakuwa ni mfano bora katika shughuli zao zote na watu. Sitaki mtu yeyote awe ni sehemu ya Jamaat hii ambaye tabia zake ni za mashaka mashaka, au ana aina nyingine yoyote ya uchafu. Hivyo kama tukipata lalamiko dhidi ya yeyote kwamba kwa makusudi anaacha majukumu yake kwa Allah, au ni sehemu ya mikusanyiko michafu au kama ana aina nyingine za tabia mbaya basi ataondolewa katika Jamaat yetu. Shamba ambalo limeandaliwa kwa juhudi kubwa kabisa na baadae mimea yake inamea, miongoni mwao kunapatikana baadhi ya nyasi pia ambazo zinapaswa kuondolewa. Kama hivyo mfanyiko wa aina hiyo wa kiasili umewekwa. Lakini Jamaat yetu kamwe haiwezi kuangamizwa na ninajua kwamba watu ambao kweli ni sehemu ya Jamaat yetu mioyo yao imefinyangwa na Allah kwa namna ambayo kwamba kwa ukweli wanajizuia na maovu na wanapenda uchaMungu. Na ninategemea kwamba wataacha mfano mzuri kwa watu wengine.

Allah Atusamehe madhambi yetu na Atushushie baraka Zake. Allah Atufanye tushuhudie mafanikio yaliyokadiriwa kwa Jamaat ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Allah Aujaalie mwaka ujao uwe wa baraka tele na mipango ya maadui isifanikiwe. Ameen.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rabiu Thani 1438 AH | JANUARI 2017 | Sulh 1396 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Dharr r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alimwambia: Usiudharau wema wowote ule hata kukutana na nduguyo kwa uchangamfu. (*Muslim*).

Kumalizika na kuanza kwa mwaka kutupatie tafakuri - Khalifa Mtukufu

Na Mwandishi Wetu,

Dar es Salaam

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alitoa hotuba katika msikiti wa Baitul Futuh mjini London, ambapo aliwakumbusha wanajumuiya kwamba kumalizika na kuanza kwa mwaka kutupatie nafasi ya kujirekebisha zaidi.

Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema:

Mwaka mpya InshaaAllah utaanza siku mbili zijazo. Sisi Waislamu tunaanza mwaka mpya kwa kutumia kalenda ya kimwezi na pia kalenda ya kijua. Hesabu ya mwaka inayotumia mwezi haifuatwi na Waislamu tu bali tangu zama za kale ilifuatwa na mataifa mengi kama vile Wachina na Wahindu. Inaonekana kutumika katika dini nyingi pia. Kabla ya Islam Waarabu walitumia kalenda ya kimwezi kuhesabu idadi ya siku. Duniani leo kalenda ya kijua inatumika zaidi na hivyo karibu kila taifa na kila nchi imeamua kuitumia hiyo katika kuhesabu siku.

Hivyo kwa kufuata hiyo Disemba 31 ni siku ya mwisho wa kila mwaka na Januari 1 inasherehekewa kama siku ya kuanza mwaka mpya. Hata hivyo, miaka inakuja, miezi kumi na mbili inapita ama iwe kwa hesabu ya kimwezi au kijua lakini watu wa kidunia hutumia siku zao, miezi yao na miaka yao kwa mambo ya kidunia na starehe za kidunia tu.

Watu hukesha usiku kucha wakipitisha muda wao kwa sherehe na kunywa pombe. Hivyo siku ya mwisho ya mwaka huagwa kwa maovu na ile ya mwanzo hukaribishwa kwa maovu. Watu walio wengi hawajali maswala ya dini hivyo hawawezi kutarajiwa kufikia vile viwango ambavyo mwaminio wa kweli anaweza kuvifikia. Adhama ya mwaminio wa kweli haimo katika kukata kwake tamaa juu ya hali hii ya dunia tu bali hasa ni kujitathmini na kujikagua juu ya mwaka uliopita. Ni kipi tumepata na kipi tumekikosa katika mwaka huu?

Sisi Waahmadiyya ni wenye bahati kwamba kwa kumfuata Masihi Aliyeahidiwa a.s. Allah ametupatia maelezo ya muhtasari wa mafundisho Yake na mafundisho ya Mtume Wake s.a.w. na Ametuonyesha viwango vya hali ya juu kabisa ambavyo kupitia hivyo tunaweza kutathmini matendo yetu na hali zetu za kiroho. Iwapo viwango hivi vitawekwa kwenye mizani basi kwa hakika tutaweza kufikia viwango vya kuwa waumini wa kweli kabisa.

Kila Ahmadiyya amechukua Bait na kupitia hiyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametupatia masharti ya kufuata na pia alitarajia kutoka kwa kila Ahmadiyya kujitathmini mwenyewe kila siku, kila wiki, kila mwezi na kila mwaka.

Lakini iwapo nasi tutajiingiza kwenye matamanio na mapenzi ya kidunia basi hapo tutapoteza mengi na hatutopata chochote. Iwapo madhaifu yetu bado yametuzidi nguvu na tathmini binafsi haitupatii utulivu nyoyoni basi tunahitajika tumuombe sana Allah kwamba mwaka ujao Atujaalie tusiwe miongoni mwa wale ambao wameanguka chini kiroho. Vinginevyo kila hatua yetu iwe ni kuelekea kwenye kutafuta radhi za Allah. Kila siku yetu iwe ni dhihirisho la mfano bora wa Mtukufu Mtume s.a.w. Mausiku yetu na michana yetu itumike kwa namna ambayo itatusaidia kutimiza ahadi zetu kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Ahadi ile ambayo inatuuliza: Je hatukutenda jambo lolote la kishirikina? Na hii sio shirki ile ya kuabudu sanamu tu bali sawa na kauli ya Mtukufu Mtume s.a.w.; hii ni hata shiriki ile ya kudunisha matendo mema au kutokutenda matendo mema. Je Sala zetu, Saumu zetu, kujitolea kwetu kifedha, kazi zetu za kuuhudumia ubinadamu na muda wetu tunaoutumia katika kazi za Jamaat, je vyote hivyo tulivifanya kwa ajili ya kupata radhi za Allah tu au tulivifanya

Endelea uk. 11

Mahafali ya Kidato cha Nne Ahmadiyya Sekondari Yafana

Na Mwandishi Wetu,

Dar es Salaam

Tarehe 13 November, 2016 katika eneo la Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya lililopo nje kidogo ya Jiji la Dar es salaam ambapo ndipo ilipo shule ya Ahmadiyya Sekondari - Kitonga, kulirindima hoi hoi, nderemo na vifijo katika kusherehekea kuhitimu kwa wanafunzi wa kidato cha nne. Alhamdulillahi.

Katika ukumbi yalipofanyika mahafali hayo, kulisheni Wanaume kwa wanawake, wazee kwa vijana, watoto kwa wakubwa . Alimuradi watu wa kila rika walihudhuria kushiriki hafla hiyo. Haya ni mahafali ya tatu tangu kuanzishwa kwa shule hii mnamo mwaka 2011.

Ufunguzi wa shughuli hii ulianza kwa usomwanji wa Quran tukufu iliyosomwa na Mmoja wa wahitimu Fadhlillah A. Ame na kufuatiwa na shairi zuri lililosomwa na wanafunzi wasichana wa kidato cha tatu ikiwa ni shairi la kuwaaga ndugu zao kidato cha nne.

Katika risala ya wanafunzi kwa mgeni wa heshima, pamoja na shukrani walizozitoa , walieleza changamoto kadhaa walizo kabiliana nazo katika kipindi chote cha masomo na kuomba zitatuliwe ili ndugu zao wanao baki, wapate maridhawa bora ya masomo ili kuongeza ufanisi wao.



Wanafunzi waliohitimu Kidato cha Nne 2016 Katika shule ye Ahmadiyya Kitonga wakiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya walimu wao mara baada ya mahafali.

Katika salamu zake mkuu wa shule Mwalimu Issa Kayombo, kwanza aliwashukuru wadau wote wa elimu alisema, sisi kama walimu tumefana kazi mliyotukabidhi kwa kiasi kikubwa na tunaamini Mwenyezi Mungu atabariki kazi ya mikono yetu.

Katika hili, naomba niwashukuru wadau wote wa Elimu kwa michango yao lakini kwa umuhimu niwataje kamati ya shule, Meneja wa shule, wazazi, walimu, watumishi wengine wa shule na wanafunzi kwa ushirikiano wao, lakini hasa wewe mgeni rasmi kwa jitihada zako.

Akigusia ufaulu wa shule , Mkuu wa shule alisema, kwetu ni jambo la kujivunia pale tunapoona vijana wetu wakichaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule zenye majina makubwa kama vile Iyunga, Songea girls, Loleza, Tambaza, Benjamin William Mkapa na kadhalika bila shaka ni viashiria bora vya ufaulu mzuri wa wanafunzi wetu na pia Baraka za Ahmadiyya.

Akimalizia kwa kuwaasa wanafunzi alisema, sisi walimu ni matumaini yetu makubwa sasa kuwa mtaenda kuwa mfanobora kwa jamii kwa sababu mnatoka Ahmadiyya Sekondari. Hatutegemei wasichana kuziona nyuso zenu mitandaoni, bali mkajiendeleze kusoma msiishie hapa ili tuje kupokezana vijiti katika kulitumikia taifa na Jumuiya yetu.

Pamoja na mengi aliyo yaeleza Meneja wa shule Bw, Musa Mgeleka kuhusiana na maendeleo ya ujenzi wa

Endelea uk. 10